Nipashe
Ijumaa Machi 19, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580524
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



**Mambo** muhimu ya kukumbukwa aliyofanya JPM

UKURASA 11, 14



**Mwanahabari** nguli aeleza alivyomfahamu chuo kikuu hadi kifo

UKURASA 19

**Aguero akasirika kunyimwa pasi**

UKURASA 21

# WAMLILIA

UKURASA 2




**Rais wa Afrika Kusini,** Cyril Ramaphosa


**Rais wa Marekani,** Joe Biden



**Rais wa Zambia,** Edgar Lungu


**Rais wa Burundi,** Evariste Ndayishimiye


**Rais wa Malawi,** Dk. Lazarus Chakwera


**Rais wa Kenya,** Uhuru Kenyatta


**Waziri Mkuu wa Uingereza,** Boris Johnson


**Rais wa Uganda,** Yoweri Museveni


**Rais wa Rwanda,** Paul Kagame

## Salamu zamiminika kila kona

UKURASA 3

MICHEZO MAJONZI YA WANAMICHEZO, WASANII KWA JPM UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



# Dunia yamlilia Magufuli



Spika wa Bunge, Job Ndugai akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu kifo cha Rais John Magufuli. **PICHA: BUNGE**

**Na Waandishi Wetu**

MARAIS na viongozi wakuu wa nchi mbalimbali barani Afrika na duniani, wametuma salamu za rambirambi kutokana na kifo cha Rais John Magufuli, kilichotokea juzi jioni.

Katika salamu hizo, wamemwelezea kuwa alikuwa shupavu, mzalendo na aliyeamini katika kukuza uchumi wa Afrika Mashariki.

Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, alitangaza juzi kifo cha Rais Magufuli kwa kuwa alifariki dunia katika Hospitali ya Mzena mkoani Dar es Salaam kwa maradhi ya moyo yaliyokuwa yakimsumbua kwa takriban miaka 10.

Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, akitoa salamu za rambirambi, pia alitangaza siku saba za maombolezo na kwamba katika kipindi hicho, bendera zitapepea nusu mlingoti.

Alisema mara nyingi walipokutana na Rais Magufuli walikuwa wakizungumza kuhusu maendeleo ya nchi hizo mbili.

"Ninakumbuka safari yake alipotutembelea Kenya, pamoja na yeye tukafungua barabara ya Southern Bypass na pia kwangu binafsi alinipatia heshima kubwa kwa kusisitiza lazima amtembelee mama yangu, Ngina Kenyatta, akaenda kumtembelea nyumbani na kutoa heshima kwake.

"Nami alinialika nimtembelee nyumbani kwake Chato na pia nikapata nafasi ya kumsalimia mama yake na kuongea naye. Tukalala nyumbani kwake na kuongea mengi kuhusu nchi zetu mbili na uhusiano wetu kama wanachama wa Afrika Mashariki, nimempoteza rafiki na kiongozi mwenzangu," alisema.

"Leo (jana) asubuhi, nimepata nafasi kuongea na Naibu (Makamu) wa Rais, Samia Suluhu Hassan, na kumpa pole zetu na kumhakikishia tutasimama pamoja naye na tutaendelea kushirikiana na yeye na wananchi wa Tanzania mpaka tuhakikishe, mzee wetu tumempumzisha," aliongeza.

**MUSEVENI ALONGA**

Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, katika ukurasa wake wa twitter, aliandika: "Nimesikitishwa sana na kifo cha Rais Magufuli. Alikuwa kiongozi ambaye anaongoza kwa uhalisia na aliyeamini katika kukuza uchumi wa Afrika Mashariki. Tunajumuika na Watanzania kuomboleza kifo cha mtoto wa Afrika. Roho yake ipumzike kwa amani."

Naye Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye, alieleza kusikitishwa na kifo cha Rais Magufuli na kutuma salamu za rambirambi na dua kwa serikali, familia na Watanzania kwa kumpoteza kiongozi shupavu na mzalendo wa kweli.

**RAMAPHOSA AOMBOLEZA**

Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, kupitia ukurasa wake wa twitter aliandika kuwa, amezungumza na Makamu wa Rais, Samia na kutoa salamu za pole.

Pia katika salamu hizo, alisema kuwa nchi yake inaungana na serikali na Watanzania katika kuomboleza kifo cha Rais Magufuli.

Paul Kagame, Rais wa Rwanda, aliandika katika twitter kuwa: "Tunasikitika kumpoteza kaka na rafiki yangu, Rais Magufuli. Mchango wake katika taifa lake na kwa Bara la Afrika hautasahaulika. Salamu zangu za dhati ziende kwa familia na Watanzania. Wanyarwanda wako pamoja na Watanzania katika wakati huu mgumu."

Rais wa Gambia, Adama Barrow, alisema kwa niaba ya serikali na watu wa Gambia, anaungana na watu wa Tanzania kuomboleza kwa kumpoteza Rais Magufuli.

Rais wa Somalia, Mohamed Abdullahi, aliandika: "Kwa niaba ya Serikali na taifa la Somalia, ningependa kuwasilisha rambirambi zetu kwa Tanzania kwa kumpoteza kiongozi Rais Magufuli. Tunalitakia taifa zima na serikali subra na utulivu katika kipindi hiki cha maombi na maombolezo."

**LUNGU AHUZUNIKA**

Rais wa Zambia, Edger Lungu, alisema amepokea kwa masikitiko na huzuni taarifa za kifo cha rafiki na kaka yake Rais wa Magufuli.

"Napenda kutoa salamu zangu za pole kwa familia ya Rais Magufuli na Watanzania ambao tunapakana na mila na desturi zetu zinafanana," alisema.

Alisema Rais Magufuli ni alama ya Afrika ambaye atakumbukwa kwa umahiri wake wa kuimarisha uchumi wa taifa lake na kuondoka kwake kumeacha pengo kubwa kwa bara zima la Afrika.

Naye Rais wa Malawi, Lazarus Chakela, alisema Malawi inaungana na Watanzania kuomboleza msiba huu mkubwa kwa siku 14 zijazo.

"Tunawaomba Watanzania wawe na nguvu pamoja na serikali yao katika kipindi hiki waendeleze umoja na mshikamano walio nao. Serikali ya Malawi iko tayari kutoa msaada wowote utakaohitajika baada ya kifo cha Rais Magufuli," alisema.

Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, ametoa salamu zake za pole kwa familia ya Rais Magufuli na Watanzania na kueleza kuwa Afrika inaomboleza pamoja nanyi.

Rais wa Venezuela, Nicolas Maduro, kupitia taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje, alisema nchi hiyo inaungana na Watanzania kutokana na kifo cha Rais Magufuli.

**CHINA YATOA NENO**

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje China, Zhao Lijian alisema Rais Magufuli alizingatia maendeleo pamoja na uhusiano na nchi yake.

China ilitoa rambirambi zake jana, kupitia ukurasa wa Shirika la Habari Xinhua, ikieleza kuwa Rais Magufuli alitoa mchango mkubwa na ushirikiano na China katika sekta tofauti.

"China inatoa salamu za rambirambi kwa kifo hicho salamu hizi ziende kwa serikali ya Tanzania na ndugu jamaa wa Rais Magufuli.

"Rais Magufuli alikuwa kiongozi imara, aliyelinda mshikamano na kuliinua taifa lake kiuchumi na maendeleo ya kijamii na kuungwa mkono na Watanzania," Zhao alisema.

China, kupitia taarifa hiyo, ilisema inaungana na Watanzania katika kipindi hiki ikizingatiwa historia ya urafiki wa muda mrefu kati ya nchi hizo mbili.

**UINGEREZA**

Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, katika ukurasa wake wa twitter akiwa kati ya viongozi wa kwanza duniani kutuma salamu za rambirambi aliandika, "Fikra zangu zipo na wapendwa wa Rais Magufuli pamoja na Watanzania," aliandika katika ukurasa wake wa Twitter.

**NIGERIA**

Rais mstaafu wa Nigeria, Goodluck Jonathan, ambaye amewahi kuongoza jopo la waangalizi wa uchaguzi ukiwamo wa mwaka 2015, aliandika kuwa: "Nyota moja imeondoka Barani Afrika, nimemfahamu Rais vizuri kwa sababu nimetembelea Tanzania mara nyingi na kuimarisha demokrasia."

**●Imeandaliwa na Romana Mallya na Christina Mwakangale**

# Mabalozi, taasisi kimataifa wamlilia

**Na Elizabeth Zaya**

BALOZI mbalimbali nchini na mashirika ya kimataifa zimeendelea kutuma salamu za rambirambi kutokana na kifo chake na kumkumbuka alivyowagusa enzi za uhai wake.

**UBALOZI WA CHINA**

"Tunatoa salamu za pole za dhati kwa familia na Serikali ya Tanzania kutokana na kifo cha Rais John Magufuli. Alikuwa kiongozi mashuhuri na mtetezi shupavu katika masuala ya kitaifa."

"Aliwaongoza Watanzania katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Dk. Magufuli alifanya mambo makubwa muhimu katika nyanja mbalimbali. Wachina tuko pamoja na Watanzania katika kipindi hiki cha huzuni."

**UBALOZI WA MAREKANI**

"Kwa niaba ya watu wa Marekani, natoa salamu zangu za pole kwa wote walioguswa na kifo cha Rais John Magufuli. Marekani tuko pamoja na Watanzania katika kipindi hiki kigumu."

**UBALOZI WA CANADA**

"Canada inatoa salamu za pole za dhati kutokana na kifo cha Rais Dk. John Pombe Magufuli. Tunaungana na familia, Makamu wa Rais na Watanzania wote kuomboleza msiba huu mzito."

**UNESCO**

"Umoja wa Mataifa Tanzania, umehuzunishwa na kifo cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Joseph Pombe. Tunatoa salamu za pole kwa serikali, familia na Watanzania wote. Apumzike kwa amani."

**UNA TANZANIA**

"Tunaungana na Watanzania wote kuomboleza kifo cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Pombe Joseph Magufuli, tunaomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi."

**WHO, AFRIKA**

"Nimeshtuka kusikia taarifa za kifo cha Mheshimiwa Rais wa Tanzania, John Magufuli, natoa salamu zangu za pole za kutoka ndani ya moyo wangu kwa familia yake. WHO tuko tayari kusaidia serikali na Watanzania katika vipaumbele vinavyohusu masuala ya afya."

**WFP**

"Kwa dhati, tumeshtuka kupokea taarifa za kifo cha Rais John Magufuli. Kutoka moyoni, tunatuma salamu zetu za pole kwa familia, marafiki na Watanzania katika kipindi hiki kigumu. Pumzika kwa amani, Rais Magufuli."

**UNFPA TANZANIA**

"Inahuzunisha kusikia kifo cha Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli, tunatoa salamu zetu za dhati za pole kwa familia na Watanzania katika kipindi hiki kigumu na cha majonzi. Apumzike kwa amani."




Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Humphrey Polepole akizungumza na waandishi wa habari na baadhi ya wanachama kwenye ofisi za CCM makao makuu jijini Dodoma jana, kuhusu utaratibu wa maombolezo ya kifo cha Mwenyekiti wa Taifa wa CCM, Rais Dk. John Magufuli. Wengine ni Katibu wa Siasa na Uhusiano wa Kimataifa wa chama hicho, Kanali Ngemela Lubinga (wa pili kulia) na (kushoto) ni Katibu Mkuu Jumuiya ya Wazazi, Erasto Sima na Katibu Mkuu wa UWT, Queen Mlozi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ndugai asema JPM alikuwa mjenga nchi

**Na Waandishi Wetu**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema Dk. John Magufuli ameiachia nchi kumbukumbu ya aina yake, akibainisha kuwa alikuwa Rais mjenga nchi.

"Hatujaweza kulala, tumepokea jambo hili la msiba wa kiongozi wetu kwa mshtuko mkubwa na majonzi makubwa hapa bungeni, Rais kwa nafasi yake ni mhimili wa pili na mdau muhimu wa Bunge," alisema Ndugai alipozungumza na waandishi wa habari bungeni jijini Dodoma jana.

Kiongozi huyo wa Bunge aliendelea: "Tumepata pigo kubwa sana, tunatoa pole nyingi kwa Makamu wa Rais, Samia Suluhu, Mama Janeth Magufuli na familia na ndugu wote kule Chato na Watanzania wote popote walipo." Alisema kutokana na wabunge kuwa kwenye ziara ya kukagua miradi ya maendeleo ya bajeti inayoishia Juni 30, mwaka huu, amelazimika kuagiza warejee Dodoma haraka baada ya kutangazwa kwa kifo cha kiongozi huyo. "Mheshimiwa Magufuli ana mambo mengi ambayo alijipambanua nayo. Alikuwa Rais mjenga nchi, hasa katika eneo la miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege, miradi mikubwa ya maji, miundombinu ya elimu, afya, bandari. Rais ameweka kumbukumbu ya aina yake," alisema.

Spika Ndugai alisema Watanzania wana jukumu la kuendeleza kwenye msingi aliouweka na malengo mbalimbali aliyoainisha kupitia hotuba alizozitoa bungeni na kuahidi kusimamia yote ikiwamo utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Wakati Spika Ndugai akiahidi hayo, baadhi ya viongozi wastaafu na mawaziri wamewasilisha salamu zao za kumlilia Rais Magufuli, wakibainisha kuwa alikuwa mchapa kazi, msema kweli na lile analolisema ndilo alilolitenda. Waziri Mkuu mstaafu, Frederick Sumaye, katika salamu zake za rambirambi alizozitoa jana, alisema taifa kumpoteza Rais aliyekuwa kwenye kiti hicho siyo jambo dogo.

Sumaye alisema alipata taarifa za msiba wa Rais kupitia runinga na hakuamini kama ni za kweli.

"Mwanzoni watu walionipigia simu, nilisema siamini kama ni za kweli, lakini sasa ninaamini ni za kweli. Ni taarifa imetushtusha sana, ni taarifa imetusikitisha sana kama taifa kwa sababu taifa kupoteza Rais ambaye yuko kwenye kiti siyo jambo dogo.

"Rais Magufuli wote tunamjua ni mchapa kazi, ni msema kweli na lile analolisema ndilo analotenda. Tumesikitika sana kumpoteza kiongozi wetu huyu, Rais wetu mpendwa lakini ndiyo kazi ya Mungu," alisema.

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, alisema: "Hayati Rais wetu mpendwa jasiri mwonyesha njia, umepigana vita vilivyo vizuri, mwendo umeumaliza na imani umeilinda. Ninatoa pole kwa Watanzania wote kwa msiba huu mzito kwa taifa, Sekta ya Habari imepata pigo."

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ummy Mwalimu, alisema: "Hakika, jambo hili ni zito na kubwa kulipokea. Ooh jemedari wetu, Rais wetu, Rais Magufuli utabaki katika mioyo yetu kama Rais jasiri, shupavu na uliyejitoa kwa ajili ya maendeleo ya Tanzania na Watanzania hususani wa kipato cha chini."

**●Imeandikwa na Romana Mallya (DAR) na Augusta Njoji (DODOMA)**

# Kamati maalum ya CCM yaitwa

**Na Waandishi Wetu**

KAMATI Kuu Maalum ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), itakutana kesho katika ofisi ndogo za chama hicho mkoani Dar es Salaam kufuatia kifo cha Rais John Magufuli.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini Dodoma, Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi wa CCM Taifa, Humphrey Polepole, alisema wakuu wa chama waliopo ambao ni Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Philip Mangula na Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Ali Mohamed Shein, wameshauriana kamati hiyo kukutana.

"Wakuu wa chama waliopo wameshauriana kamati kuu iketi kwa kikao maalum siku ya Jumamosi ya Machi 20, mwaka huu, saa nane mchana katika ofisi ndogo ya makao makuu ya CCM Lumumba jijini Dar es salaam," alisema.

Polepole pia alisema chama kitakuwa kwenye maombolezo kwa siku 21 na wakati wote bendera zitapepea nusu mlingoti na kutakuwa na kitabu cha salamu za rambirambi na maombolezi katika ofisi za chama Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar.

"Wanachama wote wa CCM na Watanzania waendelee kuwa watulivu, kusimama imara na kuendelea kutafakari mchango wa kipekee wa kihistoria wa ndugu yetu John Magufuli aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM na Rais," alisema.

Vilevile, alitangaza kusitishwa kwa shughuli za chama zinazohusu uchaguzi ndani ya chama hadi hapo yatakapotolewa maelekezo mengine.

**CHADEMA, ACT**

Wakati CCM wakitangaza hayo, Chama cha Wananchi (CUF) kupitia Mwenyekiti wake, Prof. Ibrahim Lipumba, kimesema wamepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Rais Magufuli. "Masikio yamepokea taarifa ambayo akili haziko tayari kuibeba wala kuikubali kwa kuzingatia uhalisia kwamba ni wiki tatu tu zilizopita Rais Magufuli alifanya kazi kubwa bila kuchoka za kuzindua miradi mikubwa ya Daraja la Ubungo (Kijazi Interchange) na Stendi Mpya ya mabasi Mbezi Luis," alisema.

Prof. Lipumba alisema Februari Mosi mwaka huu, Rais Magufuli alimwalika kuhudhuria maadhimisho ya Siku ya Mahakama jijini Dodoma na alimkumbusha ahadi zake alizotoa mwaka 2015 alipokuwa anazindua Bunge la 11 ikiwa ni pamoja na kukamilisha upatikanaji wa Katiba Mpya.

"Alionekana ana afya njema na mchangamfu. Alinitania kwa kusema kuwa baada ya uchaguzi nimenenepa. Aliupokea ujumbe wangu vizuri. Niliamini kabisa kiporo cha upatikanaji wa Katiba Mpya inayotokana na maoni ya wananchi atakifanyia kazi kwa dhati katika kipindi chake cha pili," alisema.

Kiongozi wa Chama cha ACT- Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema amezungumza na Makamu wa Rais, kumpa pole huku Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, akisema bendera za chama hicho zitashushwa nusu mlingoti kwa siku 21.



# Wamachinga wasema wamempoteza mtetezi



Wafanyabiashara ndogo maarufu machinga ambao ni miongoni mwa makundi yaliyokuwa yanatetewa na Rais Dk. John Magufuli, wakiwa katika shughuli zao katika eneo la Mwenge, mkoani Dar es Salaam, hivi karibuni. **PICHA: MAKTABA**

**Eliza Zaya na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAFANYABIASHARA ndogo katika eneo la Mwenge, Dar es Salaam, wamesema kifo cha Rais John Magufuli ni pigo na hawaamini kama watapata kiongozi mwingine wa kuwatetea kama yeye.

"Tunalia sisi wamachinga, Rais Magufuli ndiye alikuwa mtetezi wetu, tulikuwa tumesahau kufukuzwafukuzwa na vitu vyetu kumwagwa chini, tulikuwa tunafanya biashara kwa uhuru bila kubughudhiwa na mtu yeyote kwa sababu alituwekea kinga ilimradi uwe tu na kitambulisho chako," alisema mmoja wa wafanyabiashara hao, Kevin Kibona.

Agatha Francis, alisema kumbukumbu ya Rais Magufuli ya kuwawekea mazingira bora ya biashara, haitasahauliwa.

"Magufuli alikuwa ni rais wa wanyonge, yeye alikuwa hapendi kuona watu wa chini wanaonewa na kwa moyo wake wa kututetea tulipata nguvu ya kufanya kazi kwa bidii tukiwa na uhakika wa kutokusumbuliwa kama ilivyokuwa miaka ya nyuma," alisema Agatha.

"Alituwekea mazingira mazuri kila mahali, hata ukienda kwenye ofisi mbalimbali za serikali huduma unapata bila kusumbuliwa, bila kujali wewe ni tajiri au maskini, una fedha au huna. Alivunja kabisa makundi."

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Umoja wa Wamachinga (UMMPWA), Philemon Maliga, alisema Rais Magufuli atakumbukwa kwa kujali kundi hilo na kuomba viongozi waliobaki kufuata nyayo zake.

Alisema wamepata mshtuko wa msiba huo kwa kuwa mipango aliyokuwa ameipanga kwa ajili ya kundi hilo wanahisi kama itafutika na kuomba Waziri Mkuu kuendelea kusimamia mikakati ambayo ilipangwa kwa ajili ya kundi hilo.

Maliga alisema wataendelea kumuenzi Rais Magufuli kwa kufanya kazi kwa bidii kuifikisha nchi katika uchumi wa kati.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara Mkoa wa Pwani, Abdallah Ndauka, alisema taarifa za msiba wa Rais John Magufuli ni pigo kwao kwa kuwa alishaanza kuongoza kuelekea uchumi wa kati kwa kuwafanya wasitegemee bidhaa kutoka nje ya nchi.

Mathayo Mkayala Mwenyekiti wa CCM Kata ya Mailimoja, Wilaya ya Kibaha, alisema Rais Magufuli atakumbukwa kwa mengi aliyoyafanya ikiwamo utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo ya barabara njia sita ambazo zinapita katika wilaya hiyo kuondoa msongamano wa magari.

Aliwataka wanachama waendelee kuwa watulivu na kushikamana katika kipindi hiki cha maombolezo, pia viongozi waliopo madarakani waendelee kufuata nyayo zake kwa kuendeleza yaliyoanzishwa.






# Mbeya yatangaza maombi maalumu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KUFUATIA kifo cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, serikali mkoani Mbeya imetangaza kufanya maombi maalumu ya kumwombea pumziko la milele yatakayoshirikisha waumini wa dini mbalimbali pamoja na viongozi wa mila.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliyasema hayo jana alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu msiba huo wa kitaifa na maombi hayo yatafanyika kwenye uwanja wa mpira wa Kumbukumbu ya Sokoine.

Alisema pia maombi hayo yatalenga kumwombea Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, ili awe na ustahimilivu wa kuubeba msiba huo wa kitaifa ambao umeshtua wengi.

"Nawaomba wananchi wa mkoa wetu wa Mbeya mwendelee kuwa watulivu na kulinda amani wakati tukiendelea kuomboleza na kusubiri taratibu za mazishi na zingine za kisheria, lakini niwajulishe wananchi kwamba tumeandaa ibada maalumu itakayofanyika kesho (leo) kumwombea rais wetu pumziko la milele na lenye heri," alisema Chalamila.

Aliwataka pia wananchi kuendelea kuzingatia tangazo la Makamu wa Rais, Mama Samia la kuwa na siku 14 za maombolezo na kwamba kifo cha Rais Magufuli ni makusudi ya Mungu.

Alinukuu maandiko matakatifu kutoka katika vitabu viwili ambavyo ni Yakobo 4:1 kinachosema "Walakini hamjui yatakayotokea kesho, uzima wenu ni nini? Maana ninyi ni mvuke uonekanao kwa kitambo kisha unatoweka."

Pia kitabu cha Mhubiri 3:1 kinaeleza kwamba "Kila jambo lina majira yake, kuna kusudi la kila jambo duniani, kuna wakati wa kuzaliwa na wakati wa kufa, kuna wakati wa kupanda na wakati wa kung'oa kilichopandwa."

Baadhi ya wananchi wa Jiji la Mbeya wakiwamo wafanyabiashara wadogo maarufu 'machinga', walisema wamesikitishwa na taarifa za kifo cha kiongozi huyo ambaye alikuwa mtetezi wao mkuu.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Juhudi Mwangupila, alisema awali walikuwa wanafukuzwa na serikali kwenye maeneo mbalimbali bila kupewa maeneo mbadala ya kufanyia kazi hiyo.

Alisema baada ya Rais Magufuli kuingia madarakani walianza kutengewa maeneo maalumu ya kufanyia biashara na aliagiza viongozi wa mikoa ikiwezekana wawe wanafunga baadhi ya barabara ili machinga wazitumie kwa ajili ya biashara.

"Sisi tuliamini kwamba tumepata mtetezi, hatuwezi kukataa maana Mungu ndiye aliyetuchagulia na yeye ndiye aliyemchukua, tumeumia sana, lakini hakuna namna ya kufanya, tunamwachia yeye," alisema Mwangupila.

Aliwaomba viongozi wa serikali kuendelea kumuenzi kwa kusimamia yale aliyokuwa anayaamini ili kulileta taifa maendeleo yaliyokuwa yanakusudiwa na marehemu.

TANGAZO



# Mh. Dkt. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI
# ( 1959 - 2021 )

**Uongozi na Wafanyakazi wa Makampuni ya IPP umepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.**

**Tunatoa salamu zetu za pole kwa Makamu wa Rais Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan na Serikali yote, Mke wa Rais Mama Janet Magufuli na Familia yake, pamoja na Watanzania wote kwa ujumla.**

**Mwenyezi Mungu atupe sote uvumilivu katika kipindi hiki kigumu cha majonzi.**

**Mungu Ibariki Tanzania.**
**#RIPMagufuli**

IPP

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII



## Tuendeleze mshikamano, umoja wetu wakati huu

**TAIFA** letu limepata msiba mzito wa kifo cha Rais wa Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, kilichotokea juzi.

Tangazo la msiba huo lilitolewa juzi usiku na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ambaye alisema Rais Magufuli alikutwa na mauti hayo alipokuwa akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Mzena, jijini Dar es Salaam.

Sisi Nipashe tunatoa pole nyingi kwa serikali na familia ya Dk. Magufuli kutokana na msiba huo, huku tukiwashauri Watanzania kuendeleza utamaduni wetu wa kuvumiliana, kushikamana, kuwa wamoja, amani na kupendana.

Taarifa za msiba huo zimewagusa watu wengi ambao wamesikitishwa, kuangua vilio, mujawa na simanzi pamoja na kufadhaika. Hayo yote yanatokana na jinsi Dk. Magufuli alivyojitoa kwa ujasiri kuwatumikia wakati wote bila kuchoka kwa lengo la kulifanya taifa letu kupaa zaidi na kwa haraka kimaendeleo.

Jitihada zake hizo alizionyesha kwa vitendo tangu alipoapishwa na kuanza kutekeleza majukumu yake kama kiongozi mkuu wa serikali na dola Novemba 5, mwaka 2015, wakati wa kipindi cha kwanza kwa miaka mitano hadi alipoapishwa tena Novemba 5, mwaka jana.

Kwa wakati wote huo wa takribani miaka mitano na miezi mitatu na nusu, Dk. Magufuli alidhihirisha kwa vitendo kwamba amewapigania kweli kweli Watanzania katika kuwavusha kwenye lindi la umaskini, ambao umekuwa kikwazo kikubwa kwao.

Hatua ya katikati ya mwaka jana kwa Benki ya Dunia (WB) kuitangaza Tanzania kuingia kwenye uchumi wa kati, ni kielelezo tosha kwamba jitihada za Dk. Magufuli haikuwa kazi ya bure.

Baada ya tangazo la msiba huo, watu kadhaa wakiwamo wanafunzi, wanavyuo vya elimu ya juu, wamachinga walianza kupaza sauti za kumlilia, huku wakionyesha wasiwasi kama mambo makubwa aliyowafanyia yataendelezwa na viongozi wajao.

Ikumbukwe kwamba kumbukumbu ya makundi haya kwa kiongozi huyo ni kutokana na alivyoyasaidia kwa kutoa elimu bila malipo kwa elimu ya msingi na sekondari, mikopo kwa elimu ya juu na kuwatetea wafanyabiashara wadogo kutobughudhiwa.

Wapo pia Watanzania wengine wengi ambao wanaguswa na mambo mengi na makubwa ya maendeleo ambayo yamefanywa na Dk. Magufuli. Sio rahisi kuyataja yote kwenye safu hii, lakini kwa kutaja baadhi ni miradi ya miundombinu ya barabara, reli, usafiri wa anga (kununua ndege), afya, elimu, maji, umeme, kupiga vita rushwa na kudhibiti ujambazi.

Kazi kubwa aliyoifanya na kuibadilisha nchi ndani ya muda mfupi imemjengea umaarufu duniani, na ndiyo maana viongozi wengi wakuu wa nchi na serikali, mashirika na taasisi za kimataifa wametuma salamu za rambirambi kuhusiana na kifo chake.

Katika kipindi chote cha maombolezo mengi kuhusiana na alama aliyoiacha Rais Magufuli yataendelea kuelezwa kwa undani, lakini sisi Nipashe tunawashauri Watanzania kutulia, kushikamana na kuwa wamoja katika kipindi hiki kigumu.

Jambo la kutia moyo ni kuwa Watanzania wote tangu juzi wameweka kando tofauti zao zikiwamo za kisiasa na kuomboleza kwa pamoja msimba huu wa kitaifa.

Huu ni utamaduni wa kupongeza kwa sababu kumpoteza kiongozi mkuu wa taifa aliyeko madarakani ni jambo kubwa, ambalo likichukuliwa kwa mzaa linaweza kusababisha mpasuko kwa taifa, kama ilivyowahi kutokea katika mataifa mengine, kutokana na katiba zao kutoweka wazi suala la madaraka ya rais.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



## Hatuhitaji kurunzi kuona aliyoacha JPM

Na Beatrice Moses

**WAKATI** alipoingia madarakani Oktoba mwaka 2015, Rais Dk. John Magufuli, alijiwekea mikakati ya kuifanyia kazi, ikiwa ni hatua ya kutekeleza ahadi zake kwa umma.

Katika hiyo, kuna mradi kama wa Stieglers Gorge, ambao sasa unajulikana kwa jina Mwalimu Nyerere, ukizalisha megawati 2,000 za umeme.

Ni hatua ambayo inaelezwa kwamba itasaidia kuondoa kero ya upatikanaji wa nishati hivyo utasaidia kuimarisha shughuli za kiuchumi, ikiwamo kuongeza uzalishaji wa bidhaa viwandani.

Aliweka bayana kuwa mradi huo unajengwa kwa fedha za ndani na upo katika eneo la Selous, kunakotarajiwa kuiwezesha nchi kuwa na umeme wa uhakika, hivyo kuwezesha shughuli mbalimbali za uzalishaji wa bidhaa mbalimbali viwandani.

Ni mradi unaotarajiwa kugharimu dola za Marekani bilioni 2.9 sawa na shilingi trilioni 6.5 za Kitanzania.

Hatuhitaji kurudi kumulika juhudi zote alizofanya JPM katika kulifufua Shirika la Air Tanzania(ATCL) lililoanzishwa mwaka 1977, ambalo lilifıfia.

JPM alifanikisha kununuliwa ndege mpya zilizoipa hadhi shirika hilo kwa namna yake, akisema pia ndege hizo zinasaidia kuimarisha sekta ya utalii.

Elimu bure kwa Rais Magufuli, aliitangaza kuwa elimu kuanzia awali hadi sekondari kidato cha nne itakuwa bure, ahadi ambayo aliitekeleza na wananchi walishuhudia uandikishwaji wa watoto kuanza masomo ya darasa la kwanza kwa kiwango cha kushangaza.

> **Elimu bure kwa Rais Magufuli, aliitangaza kuwa elimu kuanzia awali hadi sekondari kidato cha nne itakuwa bure, ahadi ambayo aliitekeleza na wananchi walishuhudia uandikishwaji wa watoto kuanza masomo ya darasa la kwanza kwa kiwango cha kushangaza.**

Ni hatua hiyo iliyoenda sanjari na kuhakikisha madawati pia yanaopatikana kwenye shule hizo, ikiwa ni miezi kadhaa kabla ya kifo chake, aliwabana viongozi wa Wilaya ya Ubungo kujenga madarasa ili kuwanusuru wanafunzi waliokuwa wanakaa chini ya miti kwenye Shule ya Msingi King'ongo.

Novemba 20, 2015, Magufuli alipokuwa akilizindua Bunge alitangaza kuzifuta safari zote holela za nje, akibainisha kuwa zinaigharimu Taifa mabilioni ya fedha ambayo yangesaidia shughuli nyingine za maendeleo ikiwamo ujenzi barabara za lami.

Pia alisema kuwa fedha hizo pia zingetumika kuchimba visima vya majisafi na salama na kujenga zahanati au kununua dawa, ili kuondoa usumbufu wanaopata wananchi wanaokwenda kutibiwa kwenye hospitali za umma.

Alitoa mfano kuwa katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 na sehemu ya 2014/2015, takriban shilingi bilioni 356 zilitumika, ambapo aligawanya kuwa serikali kila uchao ni takriban Sh.milioni 975.34. kwa siku kugharamia safari za nje zikiwamo zisizokuwa na ulazima.

Aliwezesha kurejesha nidhamu kwenye kwa watendaji wa taasisi za umma ikiwamo kuwachukulia hatua kali viongozi wenye nyadhifa mbalimbali, ikawakumbusha kuwa cheo ni dhamana.

Alisimama kidete kutetea wafanyabiashara ndogo ndogo maarufu kama wamachinga akiwashambulia baadhi ya watendaji waliokuwa wakiwanyanyasa wafanyabiashara hao, ikiwamo kuwageuza vitega uchumi vyao.

Pia kuna mengine mengi ya watumishi na mishahara hewa, aliibua na kuidhibiti, jambo lilookoa mamilioni ya pesa za umma, ambazo zilitumika kujenga miradi ya umma, kama vile vituo vya afya.



# Undani ugonjwa uliosababisha kifo cha JPM

**Na Beatrice Moses**

WATAALAMU wamefafanua kwa kina kuhusu ugonjwa wa mfumo wa umeme kwenye moyo uliosababisha kifo cha Rais John Magufuli juzi jioni.

Kwa mujibu wa andiko la Daktari Richard Fogoro la mwaka 2019 lililopo kwenye tovuti ya https://sw.approby.com, mfumo wa umeme katika moyo ni muhimu kwa utendaji kazi wa moyo.

"Mfumo wa umeme huamua kiwango cha mapigo ya moyo, na pia huratibu na kuandaa kupigwa kwa misuli ya moyo," mtaalamu huyo anabainisha katika andiko lake hilo.

Anasema ukosefu wa mapigo kawaida katika mfumo wa umeme wa moyo unaweza kusababisha matatizo kwa kiwango cha moyo (kupiga haraka sana au polepole sana) au kuharibu kabisa kazi ya kawaida ya moyo.

"Tunaposema kuhusu ugonjwa wa moyo, watu wengi wanafikiria mishipa ya kupumua ambayo inaweza kusababisha mshtuko wa moyo au haja ya upasuaji wa kupungua. Hata hivyo, matatizo na mfumo wa umeme yanaweza kutokea hata kama misuli ya moyo wako ni ya kawaida," anafafanua zaidi.

Anasema ugonjwa wa moyo unaweza kusababisha kutofautiana katika mfumo wa umeme wa moyo, kama vile nyumba iliyoharibiwa katika kimbunga au mafuriko inaweza kuwa na matatizo na mfumo wa umeme.

"Hii ni sababu moja ya kufanya CPR na kuwa na upatikanaji wa defibrillators. Ikiwa dalili ya moyo inaweza kurejeshwa, baadhi ya mashambulizi ya moyo haya (na sababu nyingine za arrhythmias) zinaweza kuishi," anabainisha kitabibu.

Mkurugenzi wa Idara ya Magonjwa ya Moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Peter Kisenge, mwaka 2019 alikaririwa na vyombo vya habari akizungumzia kuhusu mfumo wa umeme kwenye moyo.

Dk. Kisenge alibainisha kuwa tatizo hilo linahusisha mapigo ya moyo kuwa chini ya asilimia 30, hali ambayo inaweza kusababisha mhusika kupoteza maisha ghafla.

"Tatizo hilo huwatokea zaidi wagonjwa wenye shinikizo la juu la moyo la muda mrefu, wagonjwa wanaopata mshtuko wa moyo na wenye hitilafu ya umeme wa moyo katika baadhi ya vyumba vya moyo," alisema.

Dk. Kisenge alisema kuwa watu wanaokumbwa na matatizo hayo, huwekewa kifaa maalum cha kuongeza utendaji kazi wa moyo kijulikanacho 'Cardiac Resynchronization Therapy Implantable Cardioverter Defibrillator (CRTD).

Alisema kuwa kwa mara ya kwanza taasisi hiyo ilianza kutoa tiba hiyo nchini Julai 22, mwaka 2019.

Tiba hiyo ilihusisha kuziba maeneo ambayo yanapitisha umeme wa moyo kwa wingi na kuleta shida katika moyo kwa kutumia mashine maalum ambayo ilitolewa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa ajili ya matibabu ya moyo nchini.

Alifafanua kuwa mashine hiyo ya Electrophysiology ina kazi ya kupima umeme wa moyo kama kuna mahali unapita bila kufuata njia ya kawaida, panapoonekana ndipo inatumika kuziba njia hizo.

Bingwa huyo wa matibabu ya moyo alibainisha kuwa matibabu ya kuziba maeneo yanayopitisha umeme wa moyo bila kufuata njia yake awali hayakuwa yakipatikana nchini, hali ambayo ilisababisha wagonjwa wenye shida hiyo kusafirishwa kwa ajili ya matibabu yaliyokuwa yakipatikana nje ya nchi.

Mtaalamu wa mashine ya kuchunguza, kutathmini na kutibu umeme wa moyo unaoenda kwa haraka (Electrophysiologist) kutoka Shirika la Madaktari Afrika la Marekani, Profesa Mathew Sachest, alisema madaktari wa Afrika wamekuwa wakishirikiana na wa JKCI kwa kipindi cha miaka mitatu katika kutoa tiba ya matatizo yanayohusu moyo.

**"Hii ni sababu moja ya kufanya CPR na kuwa na upatikanaji wa defibrillators. Ikiwa dalili ya moyo inaweza kurejeshwa, baadhi ya mashambulizi ya moyo haya (na sababu nyingine za arrhythmias) zinaweza kuishi," anabainisha kitabibu.**


MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

BURIANI

Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli



*Tutakukumbuka daima kwa kuhimiza suala la ulipaji kodi kwa maendeleo ya Taifa letu!*

1959-2021



**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**Mwemba B. Mwemba** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 678 DPT** - Toyota crown Athlete. Rangi: White Peal. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control **No. 9910820785165.**



**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**JOSHUA SALEHE NDABAZANIYE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA HAICE YENYE NAMBA ZA USAJILI T.467 AAA.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/143808/2021**



# MSHTUKO KIFO CHA RAIS JOHN MAGUFULI



Wakazi wa eneo la Mkimbizi, Manispaa ya Iringa, wakionyesha kusononeka baada ya kupata taarifa ya kifo cha Rais Dk. John Magufuli, jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**



Baadhi ya wananchi wakifuatilia taarifa za kifo cha Rais John Magufuli, kupitia kwenye meza ya muuza magazeti katika eneo la Ilala Karume, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE**



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Joseph Mkirikiti, akitoa salamu za rambirambi kwa kifo cha Rais John Magufuli, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisi kwake Mjini Babati, jana. **PICHA: GIFT THADEY**



Baadhi ya wananchi wa Jiji la Arusha, wakifuatilia maombolezo ya kifo cha Rais Dk. John Magufuli, kupitia matangazo ya runinga jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**



Baadhi ya viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Dodoma, wakijadiliana kuhusu taarifa za kifo cha Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho, Rais Dk. John Magufuli, walipokutana na Mwenyekiti wa CCM wa mkoa huo, Godwin Mkanwa (wa tatu kushoto), nje ya ofisi za makao makuu ya chama jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Humphrey Polepole akizungumza na waandishi wa habari na baadhi ya wanachama kwenye ofisi za CCM makao makuu jijini Dodoma jana, kuhusu utaratibu wa maombolezo ya kifo cha Mwenyekiti wa Taifa wa CCM, Rais Dk. John Magufuli. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Sababu mapato ya uwekezaji NSSF kupaa

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, ameieleza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na sheria kuwa mapato katika uwekezaji ya mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), yameongezeka kutoka asilimia 3 hasi (-3) hadi asilimia 4.7 chanya.

Ameeleza kuwa faida hiyo imeongezeka baada ya NSSF kutekeleza maagizo ya serikali ya kuhakikisha miradi ya kimkakati inakamilika na inaleta tija.

Katika kutekeleza sera yake ya uwekezaji, shirika linawekeza katika maeneo mbalimbali, ikiwamo dhamana za serikali, hati fungani za kampuni, mikopo, hisa katika kampuni mbalimbali, miundombinu na uwekezaji katika miliki. Kama sehemu ya uwekezaji katika miliki, mfuko unatekeleza miradi mbalimbali ikiwamo miradi ya ujenzi wa majengo.

Akizungumza wakati akiiongoza kamati hiyo, ilipokuwa ikikagua utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa majengo wa NSSF katika maeneo ya Mtoni Kijichi, Dungu, Toangoma na Mzizima, Dar es Salaam juzi, Waziri Mhagama alibainisha kuwa faida hiyo imeongezeka baada ya serikali na mfuko huo kuamua kutumia njia mbadala ya kutengeneza matumizi mbadala ya majengo ya NSSF katika miradi, matumizi ya mifumo ya TEHAMA, mabadiliko ya menejimenti pamoja na watendaji wa mfuko huo kuongozwa na uzalendo na bidii katika kutekeleza majukumu yao.

"Tunaendelea kupima uendelevu wa mfuko huu ili kuhakikisha unaleta tija kwa wanachama na Taifa pia. Tumejiridhishwa na jitihada za serikali zinasaidia mfuko kukua kwani thamani ya mfuko kwa mwaka 2018 ilikuwa Sh. trilioni 3.2 na kwa mwaka 2020 imeongezeka hadi shilingi trilioni 4.8. Makusanyo ya michango ya NSSF kwa mwezi kwa mwaka 2018 yalikuwa ni wastani wa shilingi bilioni 60, na sasa ni wastani wa bilioni 100, na hii ni sehemu moja tu ya makusanyo ya michango ya wanachama. Daraja la Kigamboni kwa mwaka 2018 lilikuwa linakusanya wastani wa shilingi milioni 650 kwa mwezi, lakini kwa sasa makusanyo ni takribani bilioni 1.2 kwa mwezi," alisisitiza Mhagama.

Aliongeza kuwa sababu ya mfuko huo kujishughulisha na masuala ya uwekezaji ni kwa sababu ya hitaji la kuhifadhi michango sehemu salama kwa faida ya leo, kesho na baadaye ili wastaafu waweze kulipwa kwa mujibu wa sheria.

Aidha, alisema mfuko huo unalo jukumu la kuandikisha wanachama wengi, kukusanya michango kwa wanachama na kuhakikisha michango hiyo inatumika katika uwekezaji.

Aliihakikishia kamati hiyo kuwa serikali itatekeleza ushauri wao kwa kuwa serikali imepewa jukumu kwenye ibara ya 11 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutengeneza mifumo itakayohifadhi Watanzania.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Najma Murtaza Giga, alisisitiza kuwa kamati imeridhishwa na utekelezaji wa miradi hiyo ambayo uratibu wake kwa upande wa serikali unasimamiwa na Waziri Mhagama, hivyo kutaka kuhakikisha miradi hiyo inakuwa endelevu ili malengo yaliyokusudiwa yafikiwe.Baadhi ya wajumbe walipongeza uwekezaji uliofanywa na NSSF, huku wakishauri kuwa uwekezaji huo uliofanywa vizuri na NSSF kwenye miradi ya ujenzi wa majengo ni vyema ukafanywa pia kwenye ujenzi wa viwanda.

Aidha, walibainisha kuwa kuwekeza kwenye viwanda, kutasaidia kuharakisha kufanikisha adhima ya serikali ya kuijenga Tanzania ya viwanda.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, William Erio, aliihakikishia kamati hiyo kuwa ushauri wao watautekeleza.

Amefafanua kuwa suala la uwekezaji kwenye viwanda wataendelea kulitekeleza kwa kuwa NSSF inatekeleza uwekaji kwenye viwanda katika mpango kazi wake waliouanza kuutekeleza tangu Julai 2020.




Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro pamoja na viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Lindi, wakifurahia utendaji kazi wa mashine ya kuchakata magogo iliyotolewa na Serikali ya Tanzania na Finland kupitia mradi wa kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu (FORVAC), iliyogawiwa kwa wakazi wa wilaya ya Nachingwea na Ruangwa, mkoani humo, juzi. PICHA: CHRISTINA HAULE

# Mfanyakazi wa kampuni ahukumiwa kwa rushwa

Na Said Hamdani, LINDI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, imemhukumu mfanyakazi wa Kampuni ya FOVARC Tanzania Ltd, Albeto Joseph, kutumikia kifungo cha miaka miwili gerezani au kulipa faini ya Sh. 600,000, baada ya kupatikana na hatia ya kutoa rushwa kwa Mtendaji wa Kijiji cha Maonga, Abdu Abdallah Licho. Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya hiyo, Elasto Phili, baada ya mshtakiwa kukiri kosa lililokuwa linamkabili, huku Licho (53) akikana kosa na shauri lake limepangwa kusikilizwa Machi 30, mwaka huu.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, mshtakiwa aliulizwa kama anazo sababu zitakazoishawishi Mahakama isimpe adhabu kali kwa kosa linalomkabili, aliomba imwonee huruma kwa kile alichodai hakuwa anafahamu kile alichokuwa anampatia Licho kuwa ni rushwa.

Pia alidai ana familia inayomtegemea, akiwamo mke, watoto na wazazi, hivyo iwapo atapewa adhabu kali atashindwa kuwahudumia.

Hakimu Phili akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 01/2021, kupitia kifungu cha 15 (a) na (b) Sheria ya Kuzuia Rushwa Namba 11/2007, alimhukumu kulipa faini ya Sh. 600,000, na akishindwa atumikie kifungo cha miaka miwili gerezani. Hata hivyo, alilipa faini hiyo na kunusurika kifungo.

Awali ilidaiwa na mwendesha mashtaka wa TAKUKURU Mkoa wa Lindi, Osboru Mulamuzi, alidai Februari 9, mwaka huu mchana, eneo la Rena Pub huko Liwale, mshtakiwa ambaye ni dereva wa Forvac Tanzania Limited na Licho wakiwa wanakabidhiana fedha hizo Sh. 50,000.

Mulamuzi alidai fedha hizo zilikuwa ni moja ya rushwa kwa Afisa mtendaji huyo, ili amgongee mihuri nyaraka zake alizokuwa amenunua kiwanja kwa ajili ya ujenzi.

## Mkuu wa shule ya sekondari afa ajalini

Na Stevie Chindiye, TUNDURU

MKUU wa Shule ya Sekondari Nakapanya wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, Desderius Mbeya, amefariki dunia katika ajali ya gari alilokuwa akisafiria kuacha njia na kugonga miti usiku wa kuamkia jana.

Taarifa zinaeleza kuwa abiria wawili alio kuwa nao katika gari hilo akiwamo mwalimu wa Shule ya Msingi Nakapanya aliyetambulika kwa jina la Levokatus Shija na Mapima Shaibu walinusurika kifo na kukimbizwa katika Hospitali ya Missioni ya Ndanda wilayani Masasi mkoani Mtwara kwa matibabu zaidi. Mashuhuda walisema chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi uliomfanya ashindwe kulimudu gari.

Diwani wa zamani, Kubodola Ambali, alisema ajali hiyo ilitokea katika kijiji cha Mchangani wakati wakielekea kijiji cha Mapinduzi katika Kata ya Namakmbale. Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Saimon Maigwa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba polisi wanaendelea na uchunguzi.

## Mradi wa maji wa mil. 900/- kunufaisha maelfu vijijini

Na Mohamed Saif

KERO ya ukosefu wa majisafi na salama iliyokuwa ikiwasumbua wananchi wa vijiji vya Nduguti na Maziliga wilayani Mkalama, mkoani Singida, imepatiwa ufumbuzi. Mkuu wa Wilaya ya Mkalama mkoani humo, Mhandisi Jackson Masaka, aliyasema hayo juzi kijijini Nduguti alipokuwa akizindua mradi wa maji wa thamani ya shilingi milioni 980 unaonufaisha zaidi ya wakazi 7,000.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, Mhandisi Masaka alipongeza Wizara ya Maji kwa utatuzi wa changamoto hiyo ambayo alisema ilichangia kuzorotesha maendeleo kwa wananchi wa Nduguti.

"Mradi huu ninaouzindua ni ufumbuzi wa changamoto iliyokuwa ikitukwamisha kujiletea maendeleo. Sasa hatuna kikwazo, tuchape kazi," alisema Mhandisi Masaka.Akiwasilisha taarifa ya mradi kwa Mkuu wa Wilaya, Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Mkalama, Mhandisi Antidius Muchunguzi, alisema uligharamiwa na Serikali ya Tanzania kupitia Mfuko wa Taifa wa Maji.Mhandisi Muchunguzi alisema umejengwa na Mkandarasi Nyakire Investment Ltd, na kwamba ulianza kutekelezwa Juni 2018 na ulikamilika Desemba, 2020.

Aliongeza mradi umeanza kutoa maji na wananchi wanapata maji yanayotosheleza, hata hivyo alisema wanaendelea na utoaji wa elimu kwa wananchi juu ya utunzaji wa miundombinu.

Hafla hiyo ya uzinduzi wa mradi wa maji wa Nduguti inakwenda sambamba na uzinduzi wa miradi na uwekaji wa jiwe la msingi maeneo mbalimbali kote nchini ikiwa ni kuadhimisha Wiki ya Maji mwaka 2021.

# Coca-Cola yajikita uchakataji bidhaa za plastiki

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya kuzalisha vinywaji baridi (Coca-Cola), imesema imejipanga kuhakikisha inaendelea kuchakata bidhaa za plastiki ili kulinda na kutunza mazingira.

Mwenyekiti wa kampuni hiyo, James Quincey, alisema kuna haja kwa makundi mbalimbali kushirikiana kwa pamoja kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi yanayosababishwa na uharibifu wa mazingira.

"Siku ya uchakataji plastiki duniani inayoadhimishwa Machi 18 (jana), inatupa nafasi ya kufikiria upya juu ya namna bora ya kuendeleza ustawi wa Afrika kwa kukuza uchumi wetu pamoja na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, yakiwamo pia yanayotokana na uharibifu wa mazingira na kutumia vifungashio taka kwenye mazingira," alisema Quincey.

"Kwa upande wetu, Coca-Cola Africa (CCBA), kuchakata plastiki ni kipaumbele, maono yetu ni kuwekeza katika sayansi kwenye ufungashaji ili kusaidia ufungashaji huo wa bidhaa lisiwe tatizo tena kwa ulimwengu na mazingira, tunataka kuunga mkono malengo ya usimamizi wa taka kwa serikali za mitaa kwa kufikia azma ya ukusanyaji na uchakataji wa plastiki kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030."

Alisema mfumo wa kampuni unalenga kuhakikisha kuwa asilimia 100 ya vifungashio vinakusanywa kutoka kwa wateja na kuchakatwa upya ifikapo mwaka 2025 na kutumia angalau asilimia 50 ya malighafi hayo iliyochakatwa kwenye vifungashio ifikapo mwaka 2030.

"Ufumbuzi wa kudumu kwa changamoto kama za ufungashaji wa taka unahitaji ushirikiano wa kuhakikisha kunatokea mabadiliko ya uchumi jumuishi na endelevu katika bara letu, sisi kama wadau tufanye kwa upande wetu na serikali ichangie kwa kuweka mazingira wezeshi ya kisheria ili kusaidia kuchochea uchakataji endelevu," alisema Quincey.

"Mamlaka pia zina jukumu muhimu katika kuwezesha ushirikiano wa sekta za umma na binafsi, kuweka viwango vya ufungashaji na sera ambazo zinahimiza uchumi wa uchakataji ili kujenga uchumi jumuishi kwa watu wote."

Alisema ipo haja pia kwa jamii, nchi, serikali na wasimamizi kuharakisha mabadiliko kuelekea biashara ya uchakataji huo ili kutekeleza kwa mafanikio na viwango vinavyohitajika.





Mhe. Dkt. JOHN POMBE MAGUFULI

1959 - 2021

SALAMU ZA RAMBI RAMBI

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Akiba Commercial Bank inaungana na Watanzania wote kwa ujumla katika kuomboleza kifo cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.**

Roho ya Marehemu ipate Rehema kwa Mungu na ipumzike kwa Amani.


## Masasi wasikitika kifo cha Magufuli

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WAKAZI wa Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, wameeleza kusikitishwa na taarifa ya kifo cha Rais Dk. John Magufuli, na kwamba taifa limepoteza kiongozi shapavu mwenye maono na uthubutu katika kutetea wananchi wanyonge.

Wakizungumza na Nipashe, wakazi hao walisema kuwa taifa limepata pigo kubwa kwa kumpoteza kiongozi, ambaye tangu alipochaguliwa kushika wadhifa wa ngazi ya juu wa rais, amefanya mambo makubwa ya kimaendeleo.

Juma Athumani, mkazi Kata ya Mkuti wilayani hapa, alisema baada ya kupata taarifa ya kifo cha Rais Magufuli juzi usiku alishindwa kupata hata usingizi kwa sababu ilikuwa ni vigumu kwake kuamini taarifa hiyo.

Alieleza kwamba wamesikitishwa na kifo hicho, hivyo wanaungana pamoja na taifa kwa ujumla katika kipindi hiki kigumu cha maombolezo.

Naye Fatuma Rajabu, alisema kifo cha Dk. Magufuli kimeacha majonzi makubwa kwa taifa na kwamba atakumbukwa kwa mambo aliyoyafanya hasa miradi mikubwa ya kimaendeleo.

Saidi Bakari, mkazi wa Migongo mjini Masasi, alisema Rais Dk. Magufuli amefanya mambo mazuri kwa taifa na alikuwa kiongozi alioonyesha nia madhubuti ya kuliendelea taifa.

## Neema ya maji yanukia wakazi wa Bagamoyo

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

WAKAZI zaidi ya 1,169 ambao wanaishi katika kitongoji cha Mtoni Kata ya Makurunge Wilaya ya Bagamoyo wanatarajia kuondokana na adha ya kukosa maji kwa muda mrefu, baada ya kukamilika kwa mradi wa majisafi na salama ifikapo Machi 30, mwaka huu.

Hayo yalibainishwa na Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Bagamoyo, James Kionaumela, wakati akitoa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainabu Kawawa, katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi wa mradi huo ambao unaotekelezwa na RUWASA.

Alifafanua kwamba mradi huo unatekelezwa kupitia mfuko wa maji wa NWF ambapo chanzo chake cha maji kinatokea katika maeneo ya Chalinze kutoka kwenye mradi wa maji DAWASA.

Alisema kazi zilizofanyika ni kujenga tangi la maji ambalo litakuwa na ujazo wa lita 50,000 ambalo limejengwa juu ya mnara wa mita 12, na kwamba ununuzi na ulazaji wa bomba lenye vipenyo mbalimbali wa kilometa 5.25 ambapo pia kutakuwa vituo nane kwa ajili ya wananchi kutekea maji.

Kawawa aliwapongeza viongozi wa RUWASA kwa kuunga juhudi za serikali katika kujikita zaidi kuwaondolea adha wananchi katika suala zima la upatikanaji wa majisafi na salama maeneo ya karibu na makazi.

Kawawa alisema lengo la serikali ni kuhakikisha inaweka mikakati madhubuti kwa ajili ya kuwaondolea kero ya upatikanaji wa majisafi na salama na kumtua mama ndoo kichwani pamoja na kuimarisha miundombinu ya mabomba ambayo yanatumika katika miradi hiyo. Aliwaomba wananchi kuwa walinzi wa kuutunza mradi huo ambao utaweza kusawasaidia kwa kiwango kikubwa na kuondokana na adha ya kusaka maji kwa kutembea umbali mrefu.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Pwani, Beatrice Kazimbazi, alifafanua kwamba katika Halmashauri ya Bagamoyo wameshatekeleza miradi ya maji zaidi ya tisa ikiwamo kufanya ukarabati wa miundombinu ya mabomba ili kuwafikishia huduma ya majisafi na salama wananchi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Bagamoyo, Mohamed Usinga, pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Maji Abdul Pyalla, walisema kukamilika kwa mradi huo wa maji utawasaidia wananchi mbalimbali wa maeneo hayo na mengine ya jirani kuondokana na kero ambayo walikuwa wanaipata kwa kipindi kirefu.




# Alivyong'arisha miundombinu

**Na Salome Kitomari**

MTU anaweza kutoka Kinyerezi mpaka Mikocheni au Mwananyamala na Kinondoni bila kukanyaga barabara ya vumbi. Msongamano wa magari katika maeneo mbalimbali Dar es Salaam yameanza kuwa historia.

Yote hiyo ni kwa sababu ya hatua za makusudi zilizochukuliwa kwa ajili za kuboresha miundombinu ili kuwaondolea mzigo wananchi waliokuwa wakitumia muda mrefu barabarani badala ya kufanya kazi za uzalishaji ili kuinua uchumi wao na kuongeza pato la taifa.

Kwa muda mrefu wananchi wamekuwa wakikaa barabarani kwenye magari saa nyingi hata kuchelewa kufika kazini na nyumbani baada ya kazi kwa sababu ya msongamano. Tofauti na wakati huo, hivi sasa mtu anaweza kutoka Segerea hadi Mikocheni kwa kutumia dakika 30 hadi 40 tu.

Siri kubwa ni uboreshaji wa miundombinu ya usafiri katika maeneo mbalimbali. Kutoka Ubungo hadi Kibaha barabara imepanuliwa na magari yanapita kwa urahisi. Hata barabara za mitaani zimetengenezwa kwa kiwango cha lami.

Nyuma ya yote hayo ni Rais John Magufuli ambaye ametangulia mbele za haki lakini ameacha kumbukumbu na alama kubwa katika miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege na ujenzi wa reli ya kisasa (SGR).

Licha ya kuwapo kwa mambo yaliyofanyika kwa viwango vya juu, pia katika maeneo mbalimbali nchini, ujenzi wa miundombinu ya barabara kuu na za mitaa unaendelea, ambayo imeiwezesha kwa kiasi kikubwa Tanzania kuingia uchumi wa kati.

Kuanzia mwaka 2015 hadi 2020, chini ya uongozi wake, zimejengwa barabara zinazounganisha Tanzania na nchi jirani, barabara zinazounganisha mikoa kwa kiwango cha lami na zinazokwenda kwenye maeneo yenye fursa za kiuchumi.



Mwonekano wa daraja la juu lililopewa jina la Kijazi (Kijazi Interchange), katika makutano ya Barabara za Morogoro, Sam Nujoma na Mandela, eneo la Ubungo, jijiji Dar es Salaam. **PICHA: IKULU**

## BARABARA

Katika kipindi hicho, barabara zenye urefu wa kilometa 2,624.27 zilijengwa na kukamilika kwa kiwango cha lami. Pia zingine zenye urefu wa kilometa 82.6 zimejengwa kupunguza msongamano wa magari barabara kuu zenye urefu wa kilometa 1,298.44 zinaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami.

Miradi mingine ni ukarabati wa barabara kuu zenye urefu wa kilometa 300.9 ambao umeshakamilika, jambo ambalo litaendelea kukumbukwa na Watanzania.

Katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Dodoma ambako ni makao makuu ya nchi na Arusha, barabara katika maeneo mbalimbali zimeimarishwa ikiwa ni pamoja na kujenga barabara za mchepuko.

Dar es Salaam kwa mfano, barabara za mitaani ujenzi wake umepamba moto. Mifano halisi ni Mwananyamala, Kijitonyama na Kinondoni kwa Manispaa ya Kinondoni, Buza kwa Mpalange na Kwa Limboa wilayani Temeke, Mbagala nako hakujaachwa nyuma.

Vilevile, hadi Juni, mwaka jana, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kilometa 4,856 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami katika barabara kuu na za mikoa pamoja na madaraja mapya 12, ulikuwa umekamilika.

Pia upembuzi yakinifu wa kilometa 452.3 kwa ajili ya ukarabati wa barabara kuu na za mikoa kwa kiwango cha lami ulikamilika, huku kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kilometa 3,653.13 ukiwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

## MADARAJA

Ili kuhakikisha usafiri unakuwa mzuri, suala la ujenzi wa madaraja lilipewa uzito wa kipekee. Mfano halisi ni katika mkoa wa Dar es Salaam ambapo ujenzi wa madaraja kadhaa umefanyika na kukamilika na pia unaendelea.

Katika mkoa huo, kuna daraja la Nyerere (Kigamboni) ambalo limekuwa mkombozi kwa watu waliokuwa wakihangaika muda mrefu kwenda au kutoka Kigamboni na maeneo mengine kama Kimbiji, Mji Mwema, Tuangoma, Gezaulole, Kisota na Kibada.

Watu watakumbuka pia adha waliyokuwa wakiipata kutokana na msongamano wa magari katika makutano ya barabara ya Nyerere na Nelson Mandela eneo la TAZARA na makutano ya barabara ya Morogoro, Nelson Mandela na Sam Nujoma eneo la Ubungo.

Kutokana na adha hiyo, serikali chini ya uongozi wake iliamua kujenga madaraja hayo ambayo yamepunguza tatizo la msongamano kwa kiasi cha juu. Madaraja hayo yamepewa majina ya watu maafuru kama Mfugale (TAZARA) na John Kijazi (Ubungo).

Sambamba na hayo liko daraja la Selander linalojengwa katikati ya bahari ya Hindi kuanzia eneo la Aga Khan hadi Kenyatta Drive, Oysterbay. Daraja hilo, kukamilika kwake, litapunguza kwa asilimia kubwa msongamano uliopo hivi sasa barabara ya Ali Hassan Mwinyi eneo la Selander.

Madaraja mengine makubwa ambayo katika uongozi wake yamekamilika ni Daraja la Magufuli, Magara, Mlalakua, Momba, Lukuledi II, Mara na Sibiti. Pia yako makubwa matano ambayo yako katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Madaraja hayo, mbali na Selander, ni Msingi, Wami, Kitengule na Ruhuhu. Mengine ni Kigongo-Busisi, Sukuma, Simiyu, Mkenda, Mtera, Godegode, Malagarasi Chini na Ugalla.

## VIWANJA VYA NDEGE

Kwa kipindi cha miaka mitano chini ya uongozi wake, Dk. Magufuli alihakikisha ujenzi wa viwanja vya ndege na miundombinu yake inakamilika ikiwamo ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria (Terminal III) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) na ukarabati na uboreshaji wa Uwanja wa Ndege wa Mwanza.

Pia ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Msalato jijini Dodoma uko katika hatua ya maandalizi ya kuanza utekelezaji. Viwanja vingine vinavyoendelea kujengwa ni Songea, Kigoma, Shinyanga, Sumbawanga, Tabora, Iringa na Musoma anmbavyo viko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Serikali yake iliweka mpango wa kujenga na kukarabati viwanja vingine 11 ambavyo upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umefanyika.

Dk. Magufuli alikuwa ameonyesha nia ya kuendelea kutafuta fedha za ujenzi wa viwanja saba vilivyobakia ambavyo ni Lindi, Kilwa Masoko, Singida, Tanga, Simiyu, Lake Manyara na Njombe.

# Alivyoimarisha uchukuzi




Rais John Magufuli akikata utepe kuzindua ndege mpya mbili aina ya Bombadier za ATCL, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam mwezi Septemba 2016. **PICHA: MAKTABA**

**Na Salome Kitomari**

SEKTA ya uchukuzi ni kichocheo muhimu katika uchumi wa taifa lolote. Ni sekta ambayo huwezesha watu kutoka sehemu moja hadi nyingine na pia kusafirisha bidhaa kutoka kwenye uzalishaji hadi kwenye masoko.

Katika kuhakikisha sekta hiyo inafanikiwa, Rais John Magufuli baada ya kuingia madarakani Novemba 5, 2015 moja ya sekta aliyoamua kuivalia nyuga ni uchukuzi kwa maana ya usafiri wa majini, anga, reli na nchi kavu i kwa kuboresha miundombinu ya barabara.

### USAFIRI WA MAJINI

Katika usafiri wa majini, awamu ya kwanza ya uongozi wa Magufuli, ndani ya miaka mitano hadi mwaka 2020, serikali ilikamilisha ununuzi wa vivuko vitatu ambavyo ni MV Tanga (Pangani - Bweni) mkoani Tanga, MV Kazi (Magogoni - Kigamboni) mkoani Dar es Salaam na MV Mwanza (Kigongo - Busisi) mkoani Mwanza.

Pia upanuzi wa awamu ya kwanza wa jengo la abiria upande wa Kigamboni katika Kivuko cha Magogoni - Kigamboni, Dar es Salaam ulifanywa ili kuwaondolea adha wananchi waliokuwa wakitumia kivuko hicho.

> “Kwa sasa ununuzi wa Kivuko cha Rugezi - Kisorya pamoja na awamu ya pili ya upanuzi wa jengo la abiria upande wa Kigamboni unaendelea.

Kwa sasa ununuzi wa Kivuko cha Rugezi - Kisorya pamoja na awamu ya pili ya upanuzi wa jengo la abiria upande wa Kigamboni unaendelea.

Aidha, katika kuboresha usafiri wa majini kwenye maziwa ya Victoria, Nyasa na Tanganyika, Magufuli aliahidi kwamba serikali itahakikisha unaimarishwa ikiwa ni pamoja na kukarabati meli na vivuko vilivyokuwapo na kujenga meli mpya kubwa ambazo zitakuwa na uwezo wa kubeba abiria na mizigo kwa wingi.

Katika kutekeleza hilo, tayari kumekuwa na meli mpya ambazo zimejengwa katika maziwa hayo. Katika Ziwa Victoria, kwa mfano, meli ya MV Mwanza 'Hapa Kazi Tu' yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo imeshakamilika na inafanya safari kazi mikoa ya Mwanza, Mara na Kagera.

Meli hiyo inashirikiana na MV Victoria yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na mizigo tani 200 kwa wakati mmoja wakati meli ya MV Butiana ikikarabatiwa ili kuungana na hizo kufanya huduma.

Kwa Ziwa Tanganyika, muda mrefu wananchi wamekuwa wakitegemea usafiri wa meli kongwe ya MV Liemba ambayo ilijengwa wakati wa ukoloni ambayo kwa sasa imekuwa si ya kuiamini sana katika kutoa huduma za usafiri.

Kutokana na kutambua hilo, serikali iliamua kuanza kujenga meli ya MV Amani ambayo licha ya kutoa huduma katika mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa, pia itahudumia nchi jirani za Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Burundi.

Kwa upande wa Ziwa Nyasa, kuna meli za MV Mbeya II, MV Njombe na MV Ruvuma ambazo zimeanza kufanya kazi na zimekuwa msaada mkubwa kwa usafiri wa abiria na mizigo katika mikoa ya Ruvuma, Mbeya na Njombe.

### USAFIRI WA ANGA

Wakati akiingia madarakani mwaka 2015, Rais Magufuli aliahidi kufufua Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) kwa kununua ndege mpya 11 ambapo nane zilinunuliwa chini ya uongozi wake na zinaendelea kutoa huduma.

Pia kumefanyika ufungaji wa rada nne za kuongozea ndege, ukarabati wa mnara wa kuongozea ndege katika Kiwanja cha Pemba, ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria JNIA, ukarabati wa jengo la abiria KIA, ununuzi wa magari mapya matatu (3) ya Zimamoto, na ufungaji wa mifumo ya kuongozea ndege (AGL) katika Viwanja vya Ndege vya Dodoma, Tabora na Mwanza.

Pia huduma za hali ya hewa zimeboreshwa kwa ununuzi wa rada tatu kwa ajili ya kufungwa katika mikoa ya Mtwara, Mbeya na Kigoma.

### BANDARI

Kwa upande wa bandari, katika miaka mitano alihakikisha ujenzi wa jengo la ghorofa 35 kwa ajili ya kuwaweka pamoja wadau wanaotoa huduma za kibandari, ikiwamo uboreshaji wa gati namba 1 - 4 na gati la kushusha magari.

Kazi nyingine zilizokamilika ni ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala (Ruvu), ujenzi wa Bandari ya Nyamisati, awamu ya kwanza ya ukarabati wa gati la kuhudumia mizigo ya Mwambao, ukarabati wa Mnara wa Kuongozea Meli, uwekaji wa mfumo wa ulinzi wa kisasa, mashine za kukagua mizigo na ununuzi wa mitambo ya kuhudumia mizigo bandarini.

Jitihada hizo zilisambaa pia katika Bandari ya Tanga na kazi iliyofanyika ukarabati wa maghala na gati namba 1 na 2, kuongeza kina na lango la kuingilia bandarini ujenzi wa gati la Pangani na ununuzi wa mitambo ya kuhudumia mizigo.

### USAFIRI WA RELI

Serikali ya awamu ya tano ilijizatiti kuimarisha usafiri wa reli. Katika kufanya hivyo, iliahidi kuboresha reli ya TAZARA inaendeshwa kwa ushirikiano kati ya Tanzania na Zambia.

Sambamba na reli hiyo, ilidhamiria kuboresha usafiri wa reli ya kati kati ya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma na Mwanza pamoja na Isaka hadi Kigali na kujenga reli ya kisasa ya kiwango cha kimataifa (SGR).

Katika kutekeleza hilo, ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (km 300) umekamilika kwa zaidi ya asilimia 80 na Morogoro hadi Makutupora (km 422) unaendelea.

Pia umefanyika ununuzi wa vichwa 11 vipya vya treni; ukarabati wa mabehewa 367; upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa SGR kutoka Mtwara hadi Mbambabay (km 1,000), Tanga - Arusha - Musoma (km 1,023), Kaliua - Mpanda - Karema, Tabora hadi Kigoma (km 411), Uvinza hadi Musongati (km 156), Isaka hadi Kigali (km 356) na reli ya jijini Dar es Salaam.

Vilevile, ukarabati wa reli ya Tanga hadi Moshi (km 359) umekamilika na huduma zilianza kutolewa Desemba 2019 na ukarabati wa reli ya Dar es Salaam hadi Isaka (Km 970) umekamilika kwa asilimia 86.



JPM 1959 - 2021

# Alivyofanikisha safari ya kufika Tanzania Viwanda

**Na Gwamaka Alipipi**

NIA ya Rais John Magufuli wakati wa utawala wake ilikuwa kuboresha uchumi ili Tanzania ifikie uchumi wa kati. Ili kufikia hatua hiyo, mkazo mkubwa ulikuwa ujenzi wa viwanda.

Takwimu zinaonesha kwa sasa kuna viwanda 53,876 nchini. Kati ya hivyo 251 ni vikubwa, 173 ni vya kati, 6,957 ni vidogo na 46,495 ni viwanda vidogo sana.

Siku zote za utawala wake alikuwa na imani aliyokuwa anaitanguliza kwa kusema: "Unapofanikisha uchumi wa viwanda, ina maana kwamba ni hatua ya kuagana na umaskini."

Katika utawala wake wa miaka mitano, serikali aliyoiongoza ilifanikiwa kujenga viwanda vipya takribani 8,477 ambavyo vilitengeneza ajira zipatazo 480,000 huku Mkoa wa Pwani ukiongoza kwa kujenga vingi. Kati ya viwanda hivyo, viwanda vikubwa ni 201, viwanda vya kati ni 460 viwanda vidogo ni 3,406 na viwanda vidogo sana ni 4,410.

Siyo hilo tu, bali serikali iliongeza juhudi za kufufua viwanda vya zamani na kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vipya kwa kuweka sera na mazingira rafiki.

Katika kutekeleza hilo, serikali iliagiza kila mkoa kuhakikisha unakuwa na viwanda visivyopungua 100 ambavyo vitakuwa vikizalisha bidhaa zitakazouzwa nje ya nchi na kuipatia nchi fedha za kigeni.

Katika utekelezaji wa agizo hilo, Halmashauri ya Mji wa Kibaha ilifanikiwa kujengwa viwanda vikubwa na vidogo vipatavyo 42 na viwanda vidogo sana vikiwa zaidi ya 200. Vyote vikiajiri Watanzania zaidi ya 6,000.

Katika hotuba yake ya uzinduzi wa Bunge la 12, Rais Magufuli alisema: "Tutaendeleza jitihada za kukuza sekta ya viwanda. Mkazo mkubwa tutauweka kwenye viwanda vyenye kutumia malighafi zinazopatikana kwa wingi hapa nchini (Mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi), vyenye kuajiri watu wengi, ambavyo bidhaa zake zinatumika kwa wingi Tanzania mfano nguo, bidhaa za ngozi, mafuta ya kula, sukari na saruji".

Wakati wa utawala wake wa miaka mitano, Rais Magufuli alihakikisha viwanda vilivyokufa vinafufuliwa na vingine vinajengwa sambamba na kuongeza ajira za kutosha kwa Watanzania.

Kwa mfano ndani ya miaka mitatu (2015-2017) tangu aapishwe kuwa Rais, ajira kwa Watanzania zitokanazo na viwanda ziliongezeka na kufikia 26,000, mchango wa sekta ya viwanda katika pato la taifa uliongezeka kutoka asilimia 5.2 mwaka 2015 hadi asilimia 5.5 mwaka 2017, kwamba kasi ya ukuaji wake ilikua kutoka asilimia 6.5 mwaka 2015 hadi asilimia 7.1 mwaka 2017/18.

Mbali na hilo, Serikali ya Rais Magufuli imeweza kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kujenga viwanda vidogo, vya kati na vikubwa.

Viwanda vilivyopewa kipaumbele ni vile vinavyotumia malighafi zinazopatikana hapa nchini, vinavyotoa ajira kwa watu wengi na vinavyozalisha bidhaa zenye soko hapa ndani na nje ya nchi.



Rais Dk. John Magufuli akiangalia soda zilizozalishwa na kiwanda cha Jambo Food Products Company Ltd, baada ya kukizindua mkoani Shinyanga mwezi Januari 2017. **PICHA: MAKTABA**



Rais Magufuli akiangalia shughuli za uzalishaji katika kiwanda cha sare za Jeshi Mgulani Jijini Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA**

> **"Kiwanda kingine ni cha nyama kiitwacho Meat King Ltd kilichopo eneo la Moshono mkoani Arusha ambacho kimewekeza Sh. bilioni 5.5 kwa ajili ya kusindika nyama ya ng'ombe, kuku na kondoo.**

Kadhalika, katika kipindi chote cha miaka mitano kumekuwapo na mwitikio mkubwa wa sekta binafsi kuwekeza katika viwanda.

Baadhi ya viwanda vilivyoanzishwa katika kipindi cha kuanzia Novemba, 2015 ni pamoja na; kiwanda cha kusindika maziwa cha Milkcom Ltd kilichopo Kigamboni jijini Dar es Salaam, ambacho uwekezaji wake ni Sh. bilioni 44, kina uwezo wa kuzalisha lita milioni 67.5 za maziwa kwa mwaka na kutoa ajira kwa watu 500.

Kiwanda kingine ni cha nyama kiitwacho Meat King Ltd kilichopo eneo la Moshono mkoani Arusha ambacho kimewekeza Sh. bilioni 5.5 kwa ajili ya kusindika nyama ya ng'ombe, kuku na kondoo.

Kingine ni kiwanda cha Lakairo Polybag kilichopo jijini Mwanza ambacho uwekezaji wake ni Sh. bilioni nne chenye uwezo wa kuzalisha magunia ya sandarusi milioni 10 kwa mwaka.

Kiwanda kingine ni Global Packaging kilichopo Kibaha mkoani Pwani ambacho kimewekeza Sh. bilioni nane, kina uwezo wa kuzalisha magunia ya sandarusi milioni 11.75 kwa mwaka na ajira ya watu 110. Pamoja na kiwanda cha nyama kilichopo mkoani Dodoma ambacho kinauwezo wa kuchinja ng'ombe 350 hadi 500 kwa siku.






Rais Dk. John Magufuli akiwa na aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, pamoja na viongozi wengine wakivuta utepe kuashiria uzinduzi wa Hifadhi ya Taifa ya Burigi, iliyopo Chato, mkoani Geita. **PICHA: MAKTABA**

# Atakavyokumbukwa kwa ukuzaji sekta Utalii

**Na Sanula Athanas**

KATIKA tafsiri ya nguzo kuu za uchumi wa Tanzania, utalii una nafasi kubwa. Takwimu za Wizara ya Maliasili na Utalii zinabainisha sekta hiyo sasa inachangia robo ya fedha za kigeni na asilimia 17.5 ya Pato la Taifa huku ikiajiri zaidi ya watu milioni 5.5.

Na kwa kadri mtu anapozama kuuchambua utalii, anakutana na vivutio vyake yakiwamo makundi ya wanyamapori na maeneo ya uhifadhi yaliyowekwa kisheria.

Katika miaka mitano ya uongozi wake, Rais John Magufuli aliyefariki dunia juzi jioni, alifanya mambo makubwa katika Sekta ya Utalii ambayo wadau wa sekta hiyo watamkumbuka kwa hilo.

**HIFADHI MPYA**

Serikali yake iliongeza idadi ya hifadhi za taifa kutoka 16 hadi 22 na misitu ya hifadhi ya mazingira asilia kutoka 17 hadi 19. Ongezeko la hifadhi za taifa limetokana na kupandisha hadhi mapori ya akiba ya Burigi, Biharamulo, Kimisi, Ibanda na Rumanyika - Orugundu kuwa hifadhi za taifa.

Hifadhi zilizoongezeka ni Burigi - Chato, Ibanda - Kyerwa na Rumanyika - Karagwe, sehemu

> **"Juni mwaka jana, wakati wa upitishaji wa bajeti ya serikali kwa mwaka huu wa fedha, serikali yake iliamua maduhuli ya TANAPA, NCAA na TAWA yakusanywe na Mamlaka ya Mapato (TRA).**

ya Pori la Akiba Selous kuwa Hifadhi ya Taifa Nyerere, sehemu ya Pori la Akiba Ugalla kuwa Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla na Pori la Akiba Kigosi kuwa Hifadhi ya Taifa Kigosi.

**VITA vs UJANGILI**

Takwimu za Shirika la Uhifadhi Duniani (IUCN), zinabainisha kuwa katika miaka ya 1970, Tanzania ilikadiriwa kuwa na faru 10,000 huku Hifadhi ya Taifa Serengeti pekee ikiwa na wanyama hao wapatao 700.

Hata hivyo, Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira na Wanyamapori (WWF), linabainisha kuwa Tanzania imepoteza takriban asilimia 99 ya faru weusi katika kipindi cha miaka 40 iliyopita.

Desemba mwaka jana, Ofisa Mwandamizi wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Mratibu wa Faru Kitaifa, Philbert Ngoti, alisema udhalimu wa ujangili umewakumba wanyamapori hao hata wakapungua kutoka 10,000 waliokuwapo nchini miaka ya 1970, ndani ya miaka 30 wakabaki 15 tu.

Kwa kutambua uovu huo, Dk. Magufuli, aliamua kuwashughulikia majangili na watu wote wanaofanya biashara haramu ya nyara, mazao ya misitu na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa.

Ni katika uongozi wake huo, Tanzania ilishuhudia kifo cha faru mmoja tu (Faru Fausta), tena kikatokana na ugonjwa huku idadi ya faru ikipaa hadi 190 kufikia Aprili mwaka jana huku serikali yake ikiweka lengo la nchi kuwa na wanyama hao 205 kufikia mwaka 2023, kwa mujibu wa Ngoti.

Mafanikio hayo yametokana na uamuzi wa serikali kuanzisha Jeshi la Uhifadhi ambalo kwa mujibu wa Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), John Nyamhanga, limepunguza vitendo vya ujangili nchini kwa kiwango kikubwa.

Kamishna Nyamhanga anabainisha kuwa katika miaka minne iliyopita, jeshi hilo lililopewa mamlaka kisheria kushughulikia na wahalifu hifadhini, lilikamata watuhumiwa 11,838 wa ujangili na maelfu ya silaha za kivita.

Chini ya uongozi wa Dk. John Magufuli, serikali ilitoa mafunzo ya utayari kwa watumishi 4,556 wa TANAPA, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) na Wakala wa Misitu (TFS) ikiwa ni utekelezaji wa kuingia kwenye mfumo wa Jeshi la Uhifadhi.

**MAPATO YA UTALII**

Kabla ya mlipuko wa virusi vya corona, Tanzania ilishuhudia kasi ya kuongezeka kwa mapato ya Sekta ya Utalii kutokana na jitihada mbalimbali zilizofanyika ikiwa ni pamoja na ununuzi wa ndege mpya za serikali na kutangaza vivutio vya nchi.

Mathalani, takwimu za wizara yenye dhamana ya utalii, zinaonyesha kuwa mapato yatokanayo na utalii wa kimataifa yaliongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 2.4 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani bilioni 2.6 mwaka 2019.

Vilevile, wastani wa siku za kukaa watalii nchini uliongezeka kutoka siku 10 mwaka 2018 hadi siku 13 kwa mwaka 2019, huku matumizi ya watalii kwa siku yakiongezeka kutoka Dola za Marekani 193 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani 266 mwaka 2019.

**UTALII KUSINI**

Ni katika uongozi wa Dk. Magufuli serikali ilianzisha mkakati wa kuendeleza na kukuza utalii katika Ukanda wa Kusini, ukizigusa baadhi ya hifadhi za taifa zikiwamo Ruaha, Udzungwa na Mikumi, kwa lengo la kusaidia kuchagiza uchumi wa wananchi wanaoishi karibu na hifadhi hizo na kuwawezesha kushiriki moja kwa moja katika shughuli za utalii.

**MIUNDOMBINU YA UTALII**

Mbali na ununuzi wa ndege, Dk. Magufuli kwa kutambua umuhimu wa Sekta ya Utalii katika uchumi wa nchi, alihakikisha serikali inaimarisha miundombinu ya barabara na viwanja vya ndege, vikiwamo vya hifadhini, huku akifungua milango kwa wawekezaji (mfano, ujenzi wa hoteli za kitalii).

**UDHIBITI WA MAPATO**

Kwa kutambua kwamba baadhi ya taasisi na mashirika ya umma yalikuwa yamekosa chombo sahihi cha kuyasimamia baada ya kufutwa kwa Tume ya Rais ya Kushughulikia Mashirika ya Umma (SCOPO), Dk. Magufuli aliamua kumulika mapato na matumizi ya taasisi na mashirika yote ya umma, akiagiza fedha zao zote ziwekwe kwenye akaunti maalum katika Benki Kuu (BoT).

Juni mwaka jana, wakati wa upitishaji wa bajeti ya serikali kwa mwaka huu wa fedha, serikali yake iliamua maduhuli ya TANAPA, NCAA na TAWA yakusanywe na Mamlaka ya Mapato (TRA).

Kimsingi, uamuzi huo si tu kwamba ulikusudia kuziba mianya ya matumizi ya ovyo, bali pia kuzinusuru mamlaka hizo zinaposhindwa kujiendesha, ikibainika kuwa baada ya mlipuko wa corona, zilishindwa kuwalipa mishahara wafanyakazi wake zaidi ya 3,000.





# Mahenge afunda TANROAD, TARURA

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ameutaka Wakala wa Barabara (TANROAD) Mkoa wa Dodoma na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kujenga utaratibu wa kuwa karibu na makandarasi waliopewa miradi katika maeneo yao ili miradi hiyo itekelezwe kwa viwango na kwa wakati.

Dk. Mahenge alitoa maagizo hayo jijini Dodoma wakati wa kikao cha Bodi ya Barabara Mkoa wa Dodoma kutathmini utekelezaji wa bajeti na namna ya kuboresha bajeti mpya 2021 hadi 2022.

"Mimi nimepita katika miradi hiyo, nimeona makandarasi wapo site (eneo la kazi) na maeneo mengi wametengeneza, lakini mvua zimeharibu na ukizingatia serikali imeshatoa fedha hakuna fedha nyingine mkandarasi asimamiwe akarabati kwenye uharibifu," alisema Dk. Mahenge.

Alisema taasisi hizo ni muhimu katika kuunganisha mikoa, wilaya, vijiji na mitaa hivyo ni vyema viongozi wa taasisi hizo kufanya kazi kwa weledi kuhakikisha wananchi wanaunganishwa na mawasiliano ya barabara ili kujikwamua kiuchumi.

Aidha, aliitaka TARURA kujenga utaratibu wa kutembelea halmashauri husika kabla ya kutenga bajeti au kuainisha barabara za kukarabati ili wapate mahitaji halisi kutoa kwenye halmashauri husika na uhitaji na umuhimu wa barabara kabla ya kuzitengea bajeti barabara hizo.

"TARURA muende kwenye halmashauri husika huko mtajua mahitaji halisi ya halmashauri hizo wao watawaambia barabara ipi ni muhimu sana kwa kipindi hicho kuliko ninyi kupanga tu bajeti bila kujua sehemu zenye mahitaji sana," alisema.

Alitaka ahadi zote za viongozi wa kitaifa ziainishwe kwa pamoja na zipewe kipaumbele na msukumo ili fedha hizo ziweze kutengwa na ahadi hizo zitimizwe.

Pia, aliwataka viongozi wa ngazi zote katika halmashauri za Mkoa wa Dodoma kuwa wasimamizi wa miradi yote inayotekelezwa katika maeneo yao.

Kwa upande wake, Kaimu Meneja wa TANROAD Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Salome Kabunda, akieleza utekelezaji wa miradi ya TANROAD alisema kwa mwaka wa fedha 2019/20 walitengewa zaidi ya Sh. bilioni 18 kwa matengenezo na ukarabati wa barabara mbalimbali.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2020 na 2021 pia walitengewa zaidi ya Sh. bilioni 18 kwa matengezezo ya barabara kuu na barabara za mkoa huku ikiwa imesaini jumla ya miradi 37 ya barabara ikiwa na ujenzi wa madaraja makubwa.

Mratibu wa TARURA Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Lusako Kilembe, alisema TARURA inajumla ya barabara zenye urefu wa kilomita 6,996.25 kati ya hizo 695.75 barabara za mikusanyiko, 3,403 barabara za mlisho na barabara 897 ni barabara za kijamii.



Spika wa Bunge, Job Ndugai akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu kifo cha Rais John Magufuli.
**PICHA: BUNGE**

# Shule ya uhitaji maalum yaombwa jijini

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

KUTOKANA na Dodoma kuwa na hadhi ya Jiji, Ofisa Elimu Maalumu Shule ya Msingi na Sekondari, Agnes Mwingira, ameshauri serikali kujenga shule maalumu ya sekondari ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanaofaulu darasa la saba kuingia kidato cha kwanza.

Mwingira alisema hayo alipokuwa akizungumza na viongozi mbalimbali kutoka serikali za mitaa Dodoma wakiwamo maofisa maendeleo ya jamii, mipango na uchumi, madiwani na watendaji wa kata kwenye warsha ya mfumo wa elimu jumuishi iliyofanyika jijini hapa.

Alisema kuwa kutokana na hadhi kubwa iliyotolewa na serikali kwa mkoa wa Dodoma kuwa makao makuu, ameishauri kuwapo kwa shule maalumu ya sekondari kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu wanaofaulu darasa la saba na kujiiunga na kidato cha kwanza.

Alisema kuwa shule hiyo ikiwapo itaweza kuwasaidia wanafunzi hao wenye ulemavu kielimu kwa kuwa kutakuwapo na miundombinu yao itakayozingatiwa kutokana na aina ya ulemavu wa mwanafunzi hii ni pamoja na walimu wenye taaluma ya ufundishaji.

"Ninaiomba serikali yangu tukufu kutokana na heshima kubwa tuliyopewa ya kuwapo kwa Jiji hapa Dodoma pamoja na makao makuu ya serikali, ni wakati sasa wa kuwa na shule maalumu kwa ajili ya watoto wenye ulemavu ambao wanafaulu kutoka darasa la saba na kuingia kidato cha kwanza waweze kuwa na shule yao ambayo itakayozingatiwa miundombinu yao pia," alisema.

Kwa upande wake mwanasheria wa kujitegemea Fredrick Mkatambo, akizungumza kwenye mafunzo hayo ya mfumo wa sheria wa elimu jumuishi kwa ajili ya viongozi hao wa serikali za mitaa, alisema kuwa watoto wenye ulemavu wanaofaulu masomo yao wanashindwa kuendelea na elimu kutokana na ukosefu wa miundombinu ya majengo ya shule.

Alisema kuwa kila mtoto mwenye ulemavu ana usikivu wake kwa ajili ya masilahi na mahitaji maalumu hivyo umuhimu wa kuwapo kwa majengo yao unatakiwa kuzingatiwa jijini hapa.

# Wito taasisi za utafiti kuwasaidia wafugaji

**Na Paul Mabeja,** MPWAPWA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, amezitaka taasisi za utafiti nchini kuwasaidia wafugaji ili waweze kufuga kisasa pamoja na kuzalisha mifugo yenye ubora na inayohitajika sokoni.

Kauli hiyo aliitoa wilayani hapa akiwa katika ziara kwenye Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) Mpwapwa na Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (LITA) Mpwapwa.

Naibu Waziri Gekul, alisema taasisi hizo zinatakiwa kusambaza mbegu bora, pamoja na kuwajengea uwezo wa kufuga ili waweze kufuga kisasa na hatimaye kujiingizia kipato.

Alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi inagusa kundi kubwa la Watanzania kutokana na wengi kufuga hivyo taasisi hizo zinawajibu wa kuwasaidia kufikia ndoto zao.

Pia aliwataka kuyatumia maeneo makubwa ambayo wanayo kwani yamekuwa yakichochea migogoro kati yao na wafugaji.

"Nimetembea katika taasisi hizi, lakini tatizo kubwa ni kuwa na maeneo makubwa ambayo hamyatumii na hivyo huchochea migogoro kati ya jamii inayo wazunguka na halmashauri wamekuwa wakizidi kuiomba na kuitumia ardhi hiyo sasa lazima ardhi mliyonayo muitumie kwa manufaa hamuwezi kuwa na ardhi hekta 8,000 lakini kuwa na ng'ombe 700 hii haikubaliki," alisema.

Pia aliutaka uongozi wa Taliri Mpwapwa kulipa madeni ya vibarua wanaoidai taasisi hiyo ndani ya miezi mitatu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Utafiti, Mafunzo na Ughani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Angelo Mwilawa, alisema moja ya majukumu ya taasisi hiyo ni kutafiti ng'ombe wa maziwa na wa nyama aina ya Mpwapwa Breed.

"Tunalenga zaidi kuhifadhi aina ya ng'ombe hao ambao wameonekana kufanya vizuri kwa ufagaji wa Tanzania," alisema.

Alisema taasisi hiyo ipo kwenye majaribio ya kuzalisha ng'ombe kwa kutumia viini tete ambavyo husaidia kupata ng'ombe wengi kwa muda mfupi.

Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, alisema taasisi hizo zinatakiwa kufanya utafiti unaolenga kumnufaisha Mtanzania wa chini ili apate faida katika ufugaji wake.

"Lazima taasisi za Mpwapwa zitumie fursa ya makao makuu Dodoma kuweza kuzalisha kwa wingi bidhaa za mifugo kama maziwa, kuku na kuwa na bucha za kisasa ambazo zitakuwa chanzo cha mapato kwa taasisi hizo na hivyo kiziwesha kujiendesha na kupunguza utegemezi kwa serikali.





# TFS kutafiti maji ya Mto Mlowo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI kupitia Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, inakusudia kufanya utafiti ili kubaini yanakotokea maji ya Mto Mlowo ambao haujulikani unakoelekea baada ya kuzama kwenye maporomoko yaliyoko kwenye Msitu wa Hifadhi wa Mwambalizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Hayo yalisemwa juzi na Meneja wa TFS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Cosmas Ndakidemi, alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusiana na uhifadhi wa Msitu huo wa Mwambalizi pamoja na misitu mingine.

Alisema baada ya kufanya utafiti huo, watafanya utaratibu wa kuyatangaza maporomoko ya mto huo kuwa miongoni mwa vivutio vya utalii katika ukanda huo.

Alisema zipo nadharia mbalimbali zinazohusiana na mto huo na hivyo ili kuzifanya ziwe za kweli lazima utafiti ufanyike wa kina na hivyo wakala huo unaendelea na mchakato huo.

"Tumeshaanza hatua za awali za kuufanyia utafiti mto huo, ili tujuwe unakoelekea baada ya kuzama kwenye maporomoko hayo, tukishamaliza tutayatangaza maporomoko hayo kama kivutio cha watalii," alisema Ndakidemi.

Hata hivyo, aliwataka wananchi wote wanaoishi kuzunguka msitu huo, kuhakikisha wanatunza mazingira ya msitu huo wa Mwambalizi ili mto huo uendelee kuwapo na kwamba utakuwa na manufaa makubwa kwao baadaye.

# Daladala zarejea baada ya siku tatu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HATIMAYE shughuli za usafiri na usafirishaji wa abiria katika Jiji la Mbeya zimerejea baada ya mgomo wa madereva daladala uliodumu kwa siku tatu mfululizo kutatuliwa na serikali ikishirikiana na Chama cha Wamiliki wa Daladala.

Madereva daladala walianza mgomo wa kufanya kazi Machi 15, mwaka huu, wakishinikiza serikali kuziondoa pikipiki za magurudumu matatu maarufu kwa jina la bajaji kwenye njia zao wakidai kuwa zinaharibu biashara yao.

Kutokana na mgomo huo, shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi zilikwama kutokana na wananchi kushindwa kusafiri kwenda kwenye maeneo yao ya kazi kwa wakati ambapo baadhi walilazimika kutembea kwa miguu na wengine wakitumia bajaji.

Serikali ya Mkoa wa Mbeya ilitumia mbinu mbalimbali kumaliza mgogoro huo ikiwamo njia ya majadiliano na madereva hao, lakini madereva hao walikuwa hawataki kumsikiliza kiongozi yeyote isipokuwa walikuwa wanamtaka Mkuu wa Mkoa huo, Albert Chalamila, ndiye azungumze nao.

Juzi mgomo huo ulifikia mwisho baada ya kikao cha Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, wamiliki wa daladala na madereva ambapo kikao hicho kiliamua bajaji kuondolewa kwenye njia zinazotumiwa na daladala.

Baada ya maamuzi ya kikao hicho, gari la matangazo la Halmashauri ya Jiji la Mbeya, lilizunguka katika maeneo mbalimbali likitangaza kuhusu uamuzi uliofikiwa na serikali.

"Hili ni tangazo maalumu la Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, bajaji zote zinatakiwa kutolewa kwenye barabara kuu na kwenye kituo cha daladala cha kabwe, pia madereva wa daladala mnatakiwa kurejesha magari barabarani," lilisikika tangazo hilo la Jiji.

Baada ya tangazo hilo, madereva daladala walieleza kufurahishwa na maamuzi hayo ya serikali, huku wakiiomba iendelee kusimamia maamuzi hayo ili kuepusha migogoro isiyokuwa ya msingi kati yao na madereva bajaji.

Mmoja wa madereva hao, Daud Gwakisa, alisema mgogoro huo ulikuwa unawafanya waishi kama wakimbizi ndani ya nchi yao kwa maelezo kuwa walikuwa hawasikilizwi na viongozi wa serikali kama ilivyo kwa makundi mengine.

"Hawa wenzetu hawafuati sheria za usalama barabarani, wanachukua abiria mahali popote, unaweza ukaongozana naye akashika breki za ghafla ili achukuwe abiria na hivyo kukusababishia ajali na ndio maana hapa mjini ilikuwa vurugu," alisema Gwakisa.

Naye Shukran Adam alipongeza serikali kwa kusikia kilio chao na kuziondoa bajaji hizo akidai kuwa maisha yao yalianza kuwa magumu baada ya kuanza mgomo na serikali ikawa inachelewa kuchukua hatua.

Alisema watahakikisha wanafanya kazi kwa kufuata sheria ili kazi yao isiingie kwenye migogoro tena na makundi mengine yanayofanya shughuli zinazofanana na za kwao.

Hata hivyo, baadhi ya wananchi walisema mgomo huo uliathiri sana shughuli zao hasa biashara na afya kwa maelezo kuwa waliokuwa wanakwenda hospitalini walikuwa wanachelewa kufika.



Baadhi ya wafanyabiashara ndogo maarufu kama machinga ambao ni miongoni mwa makundi yaliyokuwa yanatetewa na Rais Dk. John Magufuli wakati wa uhai wake, wakijadiliana jambo huku wakiendelea na biashara zao katika eneo la Sokoine, jijini Mbeya, jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wabunge wakerwa makazi kupangwa ovyo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, imekerwa na mpangilio mbovu wa makazi katika Jiji la Mbeya, huku kukiwa na kasi ndogo ya umilikishaji wa ardhi kwa wananchi waliopimiwa viwanja vyao.

Kamati hiyo ilionyesha kukerwa na mpangilio huo wakati ilipokuwa inahitimisha ziara yake mkoani Mbeya baada ya kufanya ukaguzi wa mradi wa upimaji wa viwanja katika maeneo ya Iziwa na Ituha.

Mmoja wa wajumbe wa kamati hiyo, Ally Makoa ambaye ni Mbunge wa Kondoa Mjini, alisema katikati ya Jiji la Mbeya kuna nyumba zimejengwa lakini hazina hadhi ya kuwa kwenye Jiji na badala yake zilitakiwa kuwa vijijini. Alisema Jiji kwa sasa linapima viwanja vya makazi mpaka kwenye milima wakati katikati ya Jiji kuna nyumba nyingi ambazo haziko kwenye mpangilio mzuri na hivyo akawataka kufanya utaratibu wa kuboresha makazi hayo.

Makoa alisema utaratibu wa upimaji wa viwanja katika Jiji hilo utasababisha matatizo ya migogoro ya ardhi na kuanza kuomba maeneo ya hifadhi za misitu ili zipimwe kwa ajili ya makazi. "Ujenzi wa malazi haya tunayoyaona hapa katika Jiji la Mbeya ni wa kusababisha matatizo, kuna utafiti unaonyesha kuwa baada ya miaka kadhaa kila walipo watu 10, saba watakuwa wanakimbilia mjini, sasa hili jiji mnaendelea kujenga nyumba za chini ambazo zinachukua maeneo makubwa bila sababu," alisema Makoa. Hata hivyo, alisema kwenye maeneo ya malango ya kuingilia katikati ya Jiji hilo watu wanapanda mazao marefu yakiwamo mahindi ambayo yanasababisha sura ya Jiji kutokuwa nzuri.

Naye Mbunge wa Rorya, Jafary Chege, alilitaka Jiji la Mbeya kuhakikisha linapopima viwanja liweke utaratibu wa kuweka mna miundombinu mingine ikiwamo barabara za mitaa ili kuwavutia wananchi kuchangamkia viwanja hivyo. Alisema taarifa za uuzaji wa viwanja katika Jiji hilo zinaonyesha kuwa jiji hilo linabakiza Sh. 1,000 kwenye kila mita moja ya kiwanja kulingana na bei zilizopangwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, hivyo akautaka uongozi wa Jiji hilo kutumia fedha hizo kusogeza huduma.

Alisema huduma zingine muhimu zinazotakiwa kusogezwa kwenye viwanja vinavyopimwa ni maji, umeme na huduma zingine muhimu za kijamii ili wananchi watakaojenga kwenye viwanja hivyo wasianze kuhangaika tena kupata huduma hizo.

"Mnapopima viwanja lazima mvifanye viishi kwa kuhakikisha wananchi wanajenga na kuishi, njia pekee ya kuyafanya kuwa hai ni kusogeza huduma za kijamii hasa maji na umeme," alisema Chege.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Aloyce Kwezi, aliupongeza uongozi wa Mkoa wa Mbeya kwa kusimamia shughuli mbalimbali za maendeleo hasa zinazohusiana na shughuli zinazohusu shughuli za ardhi.

Alipongeza idara ya ardhi kwa kuhakikisha maeneo yanayopimwa yanaendelezwa kwa kuzingatia sheria huku akikipongeza Chuo cha Ardhi kwa kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi.



# Mwinyi ataka mfumo endelevu Red Cross

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuna umuhimu kwa Taasisi ya Red Cross kuwa na mfumo endelevu utakaowezesha kujitegemea, kudumu na kupata ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu jijini Zanzibar, alipozungumza na viongozi wa Red Cross, Tawi la Kidongo Chekundu, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema ni muhimu kwa taasisi hiyo kama ilivyo kwa taasisi zisizo za kiserikali (NGO's) kuwa na mfumo endelevu utakaowezesha kujitegemea na kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Alisema lengo la kuwapo kwa taasisi hiyo kama zilivyo NGO nyingine ni kusaidiana na serikali, hivyo inapaswa kuwa na muundo wa kujiendesha, huku akibainisha umuhimu wake mkubwa katika jamii.

"Taasisi hii ina umuhimu mkubwa katika jamii kwa vile inakabiliana na majanga, hivyo yahitajika kuwa na uwezo wa kujiendesha, lazima mtafute njia ya kuifanya taasisi iwe endelevu," alisema.

Aliitaka taasisi hiyo kujipanga zaidi na kusema moyo walionao watendaji wake ni nyenzo muhimu katika ustawi wa taasisi hiyo, hivyo akashauri kutafuta mtaalamu wa kuandika miradi ili kuiwezesha kujitegemea kipitia miradi midogo.

Aidha, alisema ni muhimu watendaji wake kupata mafunzo katika uendeshaji wa miradi hiyo, sambamba na kuwa na masoko ya kuuzia bidhaa zao na kubainisha kuwa hatua hiyo itawasaidia watendaji kujitegemea.

Dk. Mwinyi alisema kama taasisi hiyo ingekuwa tayari imepata utaalamu, ingekuwa katika nafasi nzuri ya kusaidiwa kupitia mifuko ya serikali, ukiwamo wa uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Akizungumzia suala la ajira kwa vijana wanaohudumu katika taasisi hiyo, Dk. Mwinyi alisema serikali hailengi kubagua vikundi vya vijana wanaojitolea katika suala la upatikanaji wa ajira, bali ufinyu wa nafasi hizo unatokana na uwezo mdogo wa serikali wa kuajiri.

Alisema ni wajibu wa serikali kuwajengea uwezo na kuwawezesha vijana kwa kuwapatia mafunzo na mitaji, ili hatimaye waweze kujiajiri wao wenyewe.

Alisema upatikanaji wa ajira katika vikosi vya ulinzi na usalama (Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ)) nao una changamoto kubwa kutokana na uwezo mdogo wa serikali katika kuajiri, huku kukiwa na kiwango kikubwa cha vijana wanaojitolea katika kambi mbalimbali za mafunzo.

"Wengi wa vijana hunufaika kutokana na utaalamu wanaopata kutoka kazi za ujasiriamali, hivyo kuna umuhimu wa kujengewa uwezo katika mafunzo na kuwezeshwa kwa mitaji," alisema.

Aidha, Dk. Mwinyi aliueleza uongozi wa taasisi hiyo kuwa serikali italizingatia kwa makini ombi la kupatiwa gari la wagonjwa, hivyo akautaka kujipanga katika suala la upatikanaji wa mafuta pamoja na matengenezo, pale gari hilo litakapopatikana.

Alisema serikali inathamini mchango mkubwa wa taasisi hiyo katika utekelezaji wa shughuli zake, ikiwamo sherehe mbalimbali za kitaifa pamoja na matukio ya kijamii ambapo watu wengi hawawezi kujitolea.

Naye Mratibu wa Red Cross, Said Hassan, aliomba serikali kuangalia uwezekano wa kuwapatia ajira vijana wa taasisi hiyo pale zinapotokea nafasi, hususan katika Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto, akibainisha kuwapo kwa kundi kubwa la vijana waliopata mafunzo na kuitumikia taasisi hiyo wakibaki bila kazi.

Alisema taasisi hiyo imekuwa mstari wa mbele katika kutoa mafunzo kwa jamii ili kuchukua tahadhari ya kukabiliana majanga, ikiwamo magonjwa mbalimbali ya mlipuko.

Mmoja wa viongozi wa Red Cross, Haji Mgeni, alisema pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa na taasisi hiyo, bado kuna taasisi za serikali na NGO ambazo hazijatambua umuhimu wa kuwapo kwao na kusema wamekuwa wakipata vikwazo katika utendaji wao wa kazi, hususan wakati wa sherehe za kitaifa.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, alipotembelea kukagua eneo la uchimbaji kifusi huko Jendele, Wilaya ya Kati Unguja jana. **PICHA: OMKRZ**

# Othman ashtukia athari za mabadiliko ya tabianchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, ameitaka Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira na Idara ya Mazingira Zanzibar kufanya upembuzi wa kitaalamu wa athari za mabadiliko ya tabia nchi, ili kubaini maeneo ambayo yameathirika baada ya maeneo mengi Visiwani Zanzibar kukumbwa na hali hiyo na kutishia maisha ya wakazi wake.

Makamu wa Kwanza aliyaeleza hayo alipofanya ziara ya kuzitembele au idara zilizo chini ya ofisi yake na kufanya mazungumzo na wakuu wa taasisi hizo huko Maruhubi Wilaya ya Mjini Unguja.

Alisema maeneo mengi yameathiriwa na mabadiliko ya tabianchi, hivyo kuwataka wataalamu hao kutumia uwezo wao ili kuyahami maeneo yaliyoathiriwa yakiwamo makazi ya watu, maeneo ya kilimo na fukwe.

Akitolea mfano wa baadhi ya maeneo hayo yakiwamo Kaskazini Pemba eneo la Msuka ambapo maji ya bahari yameshaingia hadi kwenye makazi ya watu na kuanza kuangusha minazi na miti mengine.

"Lakini tatizo jingine kubwa hasa kisiwani Pemba bahari imeingia maeneo ya watu na kwa hali hii ardhi yetu inaweza kupungua na wasiwasi mkubwa kama tunaweza kubakia na mikoko mitupu," alisema Othman.

Alieleza kuwa kutokana na hali hiyo Zanzibar kuna haja ya kutumia wataalamu wa ndani na nje kuongeza ardhi ya Zanzibar na kutolea mfano wa ujenzi wa kufukia bahari uliofanywa na kampuni ya Salim Said Bakhresa katika eneo la Maruhubi.

Othman alisema wakati umefika wa kujipanga na kutathmini ikiwamo kuja na mkakati ambao utaonesha mpango mzima wa kuwa na maeneo ambayo yatafanyiwa tathmini ya kimazingira kwa kuyagawa maeneo ya makazi na ukulima bila kuathiri mazingira.

Alisema bahari nayo inachukua ardhi kwa kiasi kikubwa na kuwataka wataalamu wa idara hiyo itumie na kutafuta wataalamu kwa ajili ya kuongeza ardhi ya Zanzibar kwa kile alichokieleza kuwa eneo kubwa limeathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, alisema zipo nchi ambazo ziko vizuri kwa utaalamu wa kupanga mji kwa kutumia ardhi ndogo na kuongeza ardhi kulingana na matumizi hivyo ni vyema Zanzibar kukawa na utaalamu huo badala ya kuomba msaada wa fedha.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka mkazo na mwelekeo mkubwa wa kujenga nchi kitaalamu na kuzingatia mahitaji ya baadaye kwa maslahi ya wananchi wake na kulinda na kuhifadhi mazingira yake.

Aliongeza kuwa uwapo wa mashamba ya eka bila kushughulikiwa jambo linalosababisha kuongezeka athari za mabadiliko ya tabia nchi kutokana na ardhi hiyo kufanywa jangwa kinyume cha matumizi ya awali au kujengwa nyumba zisizozingatia mpango maalum.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, Sheha Mjaja Juma, alisema idara anayoiongoza imekabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinawafanya watendaji wengine kukosa sehemu ya kufanyakazi.

Alisema ofisi hiyo ina gari moja tuu na limechakaa na linahitaji matengenezo ya mara kwa mara.

# Vituo vya utoleaji pensheni kuongezwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Abeda Rashid Abdalla, amesema serikali imekusudia kuongeza vituo vya kutolea pensheni ili kupunguza msongamano kwa wanaofika kupata huduma hiyo.

Aliyasema hayo baada ya kutembelea vituo vya kulelea watoto vilivyomo katika Mkoa wa Mjini Magharibi kuangalia zoezi la utoaji wa huduma hiyo inavyoendelea katika vituo hivyo na kupokea malalamiko kwa wazee.

Alisema wazee wamekuwa wakipata tabu kutokana na msongamano wa watu wengi katika kituo kimoja, jambo ambalo linawafanya wazee kulalamikia kuongezewa vituo vyengine vya utoaji huduma ya pensheni ili kuondoa usumbufu uliopo.

"Wazee wenyewe ndio wanajua shida wanazopata, wazee wanakuwa ni wengi nafasi ndogo wengine wanakaa maeneo ya mbali kufika kituoni ni changamoto kubwa kwa wazee hao," alisema Naibu Katibu.

Aliwataka watendaji wa kitengo cha pensheni kushirikana na masheha kuandaa mazingira rafiki kwa wazee katika vituo vitakavyoongezwa kwa ajili ya zoezi hilo.

Naye Mkuu wa kitengo cha pensheni, Jamii Zanzibar ,Aisha Abass Seif, alisema kitengo chake kimeongeza vituo vya utoaji wa huduma hiyo kutoka vituo vitano hadi kufikia saba ambavyo vitaanza kutumika mwezi ujao ili kupunguza msongamano wa wazee kufika katika kituo kimoja kufuata huduma hiyo.

Alieleza kuwa wameandaa fomu maalum za malalamiko ambazo zitatolewa kwa wananchi kupitia masheha wao na kuzifanyia kazi ili kuona huduma ya pensheni inawaweka karibu wazee pamoja na watendaji.

Kwa upande wao wazee wanaoishi katika nyumba hizo, walisema wanaridhishwa na utoaji wa huduma hiyo japo kuwa haikidhi mahitaji ya kila kitu, hivyo wameiomba serikali kuwaongezea pensheni hiyo.

Abeda alitembelea kituo cha wazee Welezo na kuwapatia vitambulisho maalum vitakavyosaidia kuwatambulisha.



# Salamu za pole

Bodi na Uongozi wa Benki ya Standard Chartered Tanzania wanaungana na taifa zima katika kuomboleza kifo cha Mhe. Rais Dr. John Pombe Joseph Magufuli.
Tumepokea kwa mshituko na masikitiko makubwa taarifa za msiba huu.

Mhe. Rais Dr. Magufuli atakumbukwa kwa kujitoa kwake kikamilifu katika kuendeleza uchumi wa nchi yetu.

Tunaomboleza na familia yake na Watanzania wote katika kipindi hiki kigumu.

Imetolewa na Uongozi,
Benki ya Standard Chartered Tanzania.

standard chartered

MAKALA

# Nilivyomfahamu John Magufuli

**Na Joseph Kulangwa**

KWA mara ya kwanza nilikutana na John Magufuli tukiwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) mwaka 1985 akisomea kozi ya Shahada ya Kwanza ya Ualimu wa Kemia na Hisabati, mimi nikisomea Ualimu wa Siasa Jamii na Lugha.

Tukawa wote hapo kwa miaka mitatu na ushei hivi, hadi tulipotunukiwa shahada zetu na aliyekuwa Mkuu wa Chuo hicho, Alhaji Ali Hassan Mwinyi akiwa pia Rais mwaka 1988.

Magufuli akiwa mpenda masihara na mtundumtundu, tukampachika jina la boara (borer), ambaye ni mtu mpenda maskhara, mkorofikorofi hivi, lakini hatukupata kumsikia katika maovu mengine.

Kwa waliokuwa UDSM katika miaka hiyo, kama Magufuli angekuwa mkorofi kupindukia au asiyekubalika katika jamii, lazima angepambana na mkono wa Mzee Punch, ambaye alikuwa usiku wa manani akibandika mabandiko ya kashfa kwenye kuta za chuo, ilimradi 'kumwadabisha' mhusika. Bahati nzuri Magufuli hakuwa mmoja wao.

Baada ya kupata vyeti vyetu, mimi wakati naripoti sekondari ya Tambaza kama mwalimu, Magufuli alikwenda kuwa Mkemia katika Chama cha Ushirika cha Nyanza mkoani Mwanza. Baada ya mimi kufundisha kwa miaka minne, mwaka 1992 nikaacha ualimu na kujiunga na uandishi wa habari nikianzia kazi Shirika la Magazeti ya Chama (CCM).

Nilipotezana na Magufuli hadi siku moja mwaka 1992 nilipokutana naye maeneo ya Karimjee, wakati huo Bunge likiketi Dar es Salaam. Nikiwa nimetumwa na mkuu wangu wa kazi (Salvatory Rweyemamu) kwenda kuandika shughuli za Bunge. Nilipotoka nje kupunga upepo, nikakutana naye akiwa na rafiki yake wa karibu sana, Apolinary Makene.

Nilisalimiana nao kwa bashasha, hasa kwa wanachuo waliopotezana kwa kipindi kirefu, tukapeana za hapa na pale na kisha akafunguka juu ya kilichompeleka pale wakati akiwa si mbunge wala mwandishi wa habari, achilia mbali ofisa wa serikali, huku akisindikizwa.

Kwa kinywa chake, akaniambia alikuwa na matatizo ya kiafya, akisumbuliwa na moyo na alikuwa akitafuta kusaidiwa na wabunge, mchango wa kumwezesha kwenda Ujerumani kwa matibabu. Tangu hapo nikajua kumbe alikuwa na tatizo kubwa.

Tuliachana siku ile, nadhani alifanikisha ile safari yake, kwa sababu sikumwona wala kumsikia tena, ingawa kuna siku nilikutana na Makene ambaye aliniambia alikuwa Rufiji kikazi, naye akasema hakuwa amewasiliana na rafiki yake huyo kwa kipindi kirefu.



Rais Dk. John Magufuli. **PICHA: MAKTABA**

Katika Uchaguzi Mkuu mwaka 1995 ambao ulikuwa wa kwanza kuhusisha vyama vingi vya siasa, Magufuli aligombea ubunge na kushinda Jimbo la Biharamulo Mashariki kwa tiketi ya CCM, akipigiwa upatu na mgombea urais wa CCM, Benjamin Mkapa, ambaye alishinda.

Baada ya Mkapa kushinda urais hakumwacha, akamteua kuwa Naibu Waziri wa Ujenzi chini ya Mama Anna Abdallah, huku duru za kisiasa zikidai kuwa Magufuli hakupenda kuwa chini ya waziri mwanamke, kwamba ni kinyume na mila za kabila lake la Kisukuma.

Zilidai alifikia hatua ya kumwona Rais Mkapa kupinga uteuzi huo, lakini akamkatalia na kumtaka aendelee na kazi. Alifanya hivyo na hatimaye kubaini kuwa alikuwa chini ya mwanamke shujaa na mchapakazi na aliyechangia kumfikisha alikofika.

Baada ya uteuzi, siku ya kuapishwa Baraza la Mawaziri Ikulu, Dar es Salaam, nilitumwa tena kuandika habari hizo. Magufuli akiwa amekaa sehemu walikokuwa mawaziri, aliponiona alisimama na kunifuata na kunikumbatia, huku nikimpongeza kwa hatua ile.

Nilijisikia vizuri sana, kwamba angalau nina aliyekuwa mwanafunzi mwenzangu katika uongozi wa juu serikalini. Hata hivyo, pamoja na kuwa na ofisi yake Dar es Salaam, sikuwa mtu wa kumfuatafuata ofisini, iwe kikazi au kirafiki.

Lakini tuliendelea kukutana hata Bunge lilipokuwa limehamia Dodoma. Mikutano ya Dodoma, ilikuwa na raha yake, kwamba kila jioni, wanahabari na wabunge walichanganyana katika vijiwe kwa nyama choma na kinywaji. Chako Ni Chako ilikuwa maarufu sana. Bila kufika hapo hujafika Dodoma.

Nakumbuka siku moja kikao cha jioni bungeni, baada ya kuona hakuna cha ziada na stori nilishatuma, nikahisi mfuko wangu mwepesi, nikajiambia mtu wa kuniongeza uzito bungeni si mwingine bali 'mate' wangu Magufuli.

Kama ilivyokuwa, hakukuwa na simu za mkononi kwamba ukimtaka mbunge umtumie ujumbe, tulizoea kuwaandikia vimemo vilivyofikishwa kwao na watumishi wa ukumbi wa Bunge.

Baada ya kuhisi wepesi wa mfuko, nikaandika kikaratasi na kumpa mhudumu, nikimwomba Magufuli tuonane nje ya ukumbi. Nilimfuatilia mhudumu kwa macho mpaka alipofika kwa Naibu Waziri na kumpa. Alipokisoma mara akasimama nami nikatoke nje tukakutana.

Alipenda sana kuniita 'ndugu yangu' au 'chikaka', alipenda sana kujifunza lugha za watu. Chikaka ni neno la Kijita lenye maana ya kijana machachari. Hivyo alipofika nje, akaniuliza: "Kutiki chikaka (Vipi kijana)?" Nikafunguka kwamba hali mbaya na nilikuwa nataka nikapate kinywaji.

Jibu alilonipa likaninyong'onyeza, kwani lilikuwa jibu katika mfumo wa swali: "Kwani ofisini hamkupewa fedha za matumizi?" Nilihisi kutaka kuanguka. Naye aliona nilivyohamanika kwa sekunde kadhaa na kama anataka kuondoka hivi, akaingia mfukoni na kuchomoa Sh 10,000, akanipa nikasahau kabisa yaliyopita muda huo. Nikaitafuta Chako Ni Chako.

Huyo ndiye Magufuli. Hakuanza kuwa mkweli leo au jana bali siku nyingi. Nyeupe aliita nyeupe na si nyeusi. Tangu siku hiyo sikurudia kosa lile, ingawa tuliendelea kuwa marafiki hasa katika mikutano hiyo ya Bunge.

Kuna nyakati ikabainika kuwa aliwekewa sumu kwenye chakula na kukimbizwa nje ya nchi kwa matibabu. Aliporejea na kuhudhuria vikao vya Bunge, tulionana siku moja akanishika mkono na kuniambia: "Twende huku ndugu yangu." Tukatoka tukaenda kukaa nje ya mgahawa wa Bunge na ndipo alipofunguka: "Ndugu yangu watu wabaya, walitaka kuniua. Tulialikwa nyumbani kwa...(anamtaja jina) wakaniwekea sumu, sijui kwa nini?"

Nilimpa pole na kumtazama nikijiuliza kwa nini kiongozi huyu ananipa siri hii, ameniamini vipi? Sikumwelewa Magufuli, nikajipa imani kwamba ananiamini sana na sikupata kulisema hili kokote mpaka anaondoka duniani, kwa sababu niliamini ningelisema ningeisumbua sana nafsi yake.

Siku nyingine usiku katika hafla iliyofanyika Ikulu, Dar es Salaam, baada ya Rais Jakaya Kikwete kuapa kuongoza muhula wa pili wa miaka mitano, nikakutana na Magufuli akiwa na mwanawe bila kinywaji wala chakula.

Nikamwuliza: "Mheshimiwa vipi mbona sikuoni na chochote mkononi?" Akanijibu: "Ndugu yangu si unajua tena, mimi kula ovyoovyo tena unadhani nataka...hukumbuki?" Tukacheka na kuchukua kila mtu njia yake.

Aliendelea na nyadhifa zake zote, hatukupata kukutana tena wala kuwasiliana, hadi alipokuja kugombea urais mwaka 2015, ndipo nikakutana naye ofisi ndogo za makao makuu ya CCM Lumumba, Dar es Salaam, akiwa tayari ameteuliwa mgombea wa CCM.

Nilisalimiana naye akanitania: "Ndugu yangu naona unaota mvi!" Nami nikamtania: "Nakuona unaota upara!" Tukacheka na kila mtu akashika lake lililompeleka pale. Yeye akienda kuzungumza na viongozi wa CCM, huku mimi nikiwa katika mikakati ya kuandaa timu ya kumsaidia katika kampeni, lakini bila yeye kujua.

Kampeni zilianza na hata yeye hakujua niko kwenye timu ya kumsaidia mpaka anapata ushindi. Pamoja na kuwa chini ya Meneja Kampeni Januari Makamba, bado Rais Magufuli mpaka anaapishwa pengine mpaka anafariki dunia, hakuwa amejua kuwa nilikuwa naye kwenye kampeni.

Hata siku anavamia ofisi za kampuni ya Uhuru Publications Limited zinazochapa magazeti ya Chama ya Uhuru, Mzalendo na Burudani pale Lumumba, nikiwa nimeshaondoka hapo muda si mrefu kabla hajaingia madarakani, aliniulizia baada ya kulalamikiwa kuwa nilikuwa miongoni mwa wafanyakazi waliokuwa wanalipwa mshahara, lakini hawako ofisini, akajibiwa nilishaajiriwa JamboLeo ya mfanyabiashara Yusufu Manji.

Kwa kuwa siku hiyo, wafanyakazi walimwomba awasaidie kulipwa mishahara yao iliyokuwa imelimbikizwa, aliwataka wamwandalie orodha na kiasi kinachotakiwa kwa kila mfanyakazi.

Baada ya kupelekwa, siku moja usiku akiwa ofisini kwake, akanipigia simu na kuniambia ameliona jina langu miongoni mwa wadai, huku akiweka maskhara kama kawaida, akichanganya na yale ya 'Hall Three' (kwa waliopitia UDSM). Lakini akaniambia kuna watu 'walimlisha tango pori' kuwa nilikuwa kambi nyingine! Akaishia kunikaribisha Ikulu na familia yangu. Lakini mpaka anafariki dunia mwaliko huo haukutimia.

Huyu ndiye Magufuli ambaye hata siku ya mahojiano maalumu na wanahabari Ikulu Dar es Salaam alitumia jina langu kuzisema shule hewa za Dar es Salaam akitumia Kulangwa International School.

Ndiye Magufuli niliyemfahamu, rafiki, mwenye msimamo, mpenda maskhara na utani mwingi, lakini msema ukweli anayemaanisha akisemacho. Kalale pema ndugu yangu rafiki wa Chikaka. Dk. John Pombe Joseph Magufuli. Ameen!

# SIMEONE: NI KAWAIDA SUAREZ KUKASIRIKA



**LONDON,** England

DIEGO Simeone amesisitiza ni "kawaida" kwa Luis Suarez kukasirika baada ya kutolewa nje wakati Atletico Madrid ikikumbana na kipigo kutoka kwa Chelsea.

Mabao kutoka kwa Hakim Ziyech na Emerson Palmieri yaliipa Chelsea ushindi wa 2-0 kwenye mchezo wa pili wa hatua ya 16 ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kufuzu hatua ya robo fainali.

Suarez aliweza kupiga shuti moja tu lililolenga goli huku akigusa mpira mara 19 kabla ya kutolewa nje na nafasi yake kuchukuliwa na Angel Correa katika dakika ya 58 pale kwenye dimba la Stamford Bridge, juzi Jumatano.

Baada ya kutoka dimbani, nyota huyo wa zamani wa Barcelona alionekana amekasirika kwa kitendo hicho.

"Ni kawaida kwa wachezaji kukasirika unapowatoa nje," alisema Simeone akiiambia Movistar.

"Tulitaka kubadili vitu pale mbele na kujaribu kutafuta njia nyingine ya mashambulizi. Sitafuti sababu ya kujitetea kwa kufungwa.

"Walistahili kushinda mechi zote mbili. Mchezo wa kwanza walipata bao na leo (juzi) wakapata mabao mengine mawili, na kwa sababu walikuwa bora walistahili ushindi."

# Arteta amtaka Odegaard kufunga zaidi

**LONDON,** England

MARTIN Odegaard ana kila kitu kuwa "mchezaji aliyekamilika" kwa mujibu wa Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, ambaye anafikiri raia huyo wa Norway anaweza kuongeza mabao zaidi.


Odegaard ameonyesha kiwango cha kuvutia tangu alipojiunga na washikabunduki hao kwa mkopo akitokea Real Madrid Januari, mwaka huu na kufuatia na bao lake la pili dhidi ya Olympiacos wiki iliyopita, huku akisawazisha kwenye mchezo wa Ligi Kuu England uliochezwa Jumapili ambao ulimalizika kwa ushindi wa 2-1 dhidi ya Tottenham.

Kuelekea mchezo wa pili wa marudiano wa Ligi ya Europa dhidi ya Olympiacos jana, ambapo wanaongoza kwa 3-1, Arteta amemsifia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22.

"Anakuwa bora na bora zaidi. Nafikiri anaelewa nini anachotakiwa kukifanya," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Anacheza vizuri. Na anafanya kazi nzuri na kwa mawazo yangu anaweza kuimarika zaidi akiwa ndani ya boxi.

"Ameshafunga mabao mawili, kwa hakika amekuwa muhimu zaidi. Lakini anatakiwa kufunga mabao zaidi ili kuwa mchezaji aliyekamilika."





# Carragher aitoa Liverpool nne bora

**LIVERPOOL,** England

JAMIE Carragher amesema haoni uwezekano wa Liverpool kutinga nne bora ya Ligi Kuu England msimu huu.

Carragher ambaye ni nyota wa zamani wa kikosi hicho kinachonolewa na kocha, Jurgen Klopp, anaiona nafasi hiyo ni finyu mno kwa mabingwa hao watetezi wa ligi hiyo.

Liverpool imekuwa kwenye mwendo wa kusuasua msimu huu, jambo ambalo linatokana na wachezaji wake wengi muhimu kuwa majeruhi.

Amesema kuwa bado anaona kuna nafasi kubwa ambayo timu hiyo imeachwa jambo litakalowafanya washindwe kumaliza wakiwa ndani ya nafasi nne za juu.

Ikiwa imecheza jumla ya mechi 29 ipo nafasi ya sita na pointi zake 46, imeachwa kwa tofauti ya pointi 25 na vinara ambao ni Manchester City wakiwa na pointi 71 baada ya kucheza mechi 30.

Carragher ameiambia BBC Sport: "Bado kuna gepu kubwa ipo ila kwa sasa siamini kama Liverpool itaingia kwenye nne bora.

"Sidhani kama kuna uwezekano huo, lazima tukubali kwamba msimu huu Liverpool haitaweza kufanya hivyo."

HABARI MICHEZO

# Napoli yashusha bei ya Koulibaly

**NAPLES,** Italia

NAPOLI imekubali kushusha bei ya beki wao kisiki na nyota wa Timu ya Taifa ya Senegal, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 29, ili kumuuza katika dirisha lijalo la majira ya joto.

Mchezaji kwa sasa anapatikana kwa pauni milioni 38 kutoka pauni 80 milioni iliyokuwa inahitajika hapo awali.

Kushushwa kwa bei hiyo kunazipa afueni Bayern Munich, Liverpool na Manchester United ambazo zimekuwa zikihitaji saini yake kwa muda mrefu.

Mkataba wa mchezaji huyo unatarajiwa kumalizika mwaka 2023.

Katika siku za hivi karibuni Munich na Liverpool ndio zinaonekana kuongeza nguvu zaidi kwenye harakati za kuwania saini ya nyota huyo kwa sababu zinahitaji akazibe mapengo kwenye safu zao za ulinzi zenye upungufu mkubwa kwa msimu huu.

Koulibaly msimu huu amecheza mechi 30 za michuano yote na amefunga bao moja.




# LEBRON JAMES ATUA LIVERPOOL




**NEW YORK,** Marekani

MCHEZAJI wa mpira wa kikapu mahiri zaidi duniani, LeBron James ameingia kwenye uwekezaji katika kampuni mama ya michezo ya Fenway Sports Group, FSG, inayomiliki timu ya kikapu Boston Red Sox na Liverpool inayoshiriki Ligi Kuu England.

FSG walitangaza Jumatano kumkaribisha nyota huyo wa kikapu kuwekeza kwenye kampuni hiyo. Lebron alikuwa na hisa katika klabu ya Liverpool tangu mwaka 2011 na ana hisa ya asilimia mbili katika klabu hiyo aliyonunua kwa pauni milioni 4.7.

LeBron na mwenza wake wa kibiashara, Maverick Carter sasa wanachukua jukumu kubwa katika umiliki wa michezo duniani.

Wawili hao wanakuwa washirika wa kwanza weusi katika kampuni ya FSG baada ya kupanua uwekezaji wao katika kampuni hiyo, ambayo ina thamani zaidi ya dola bilioni sita, kwa mujibu wa jarida la Forbes la biashara.

FSG inasonga mbele na mipango kabambe ya upanuzi na wiki hii pia imeidhinisha mpango wa uwekezaji wa kibinafsi wa dola milioni 750 na washirika wa RedBird.

Ripoti zinaonyesha FSG inaweza kutumia mtaji kununua vivutio vingine vya michezo na pia kuimarisha klabu ya Liverpool.

Sehemu ya asilimia 2 ya hisa za LeBron pale Liverpool sasa ina thamani ya zaidi ya pauni milioni 37, kwa mujibu wa tathmini ya hivi karibuni.

# Aguero akasirika kunyimwa pasi

**MANCHESTER,** England

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Sergio Kun Aguero, amewalalamikia wachezaji wenzake kwa kumnyima pasi kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Atalanta.

Aguero amekuwa nje ya uwanja kwa kipindi kirefu cha msimu huu kutokana na kuwa majeruhi na maambukizi ya virusi vya corona na kusababisha kucheza katika michezo 14 tu katika mashindano yote hadi sasa msimu huu.

Aguero aliingia katika dakika ya 75 katika mchezo dhidi ya Atalanta Jumanne kuchukua nafasi ya Bernardo Silva wakiwa wanaongoza 2-0.

Katika dakika hizo mshambuliaji hakufanikiwa kupiga shuti hata moja na mwishoni mwa mchezo alionyesha kutokuwa na furaha na wachezaji wenzie.

Baada ya mchezo akiwa anatoka alisikika akisema: "Hawataki kunipa pasi."

Na baadaye alipoulizwa na waandishi wa habari, alirudia tena kusema; "Hawataki kunipasia, nimekasirika."

Hata hivyo, Kocha wa City, Pep Guardiola, hakuwa tayari kulizungumzia hilo kwa kujibu kuwa ushindi ndio lilikuwa lengo lao kuu.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# TIMU ZINAIOGOPA CHELSEA - TUCHEL

●●● Ni kutokana na kiwango kizuri kinachoonyeshwa na timu hiyo iliyoimarika baada...

**LONDON,** England

THOMAS Tuchel anaamini hakuna anayetaka kukutana na Chelsea kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katika hatua ya robo fainali, baada ya Blues hao kuwaondoa Atletico Madrid.

**Chelsea iliwafumua vinara hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Atletico Madrid mabao 2-0 katika dimba la Stamford Bridge juzi Jumatano na kufuzu hatua ya robo fainali kwa ushindi wa jumla wa 3-0.**

Hakim Ziyech na Emerson walifunga mabao hayo ya Chelsea na kuiwezesha kufikisha mechi 14 bila kufungwa kwenye mashindano yote, na 13 tangu Tuchel alipochukua mikoba kutoka kwa Frank Lampard Januari 26, mwaka huu.

Chelsea bado haijaruhusu bao katika mechi sita za nyumbani chini ya Tuchel kwenye mashindano yote, huku Blues wakicheza bila nyavu zao kutikiswa katika mechi 11 kati ya 13 chini ya raia huyo wa Ujerumani, nyingi zaidi kuliko klabu yoyote kwenye Ligi Kuu England tangu mechi yake ya kwanza.

Kuelekea droo ya kupangwa kwa ratiba ya robo fainali leo Ijumaa, Tuchel amesema: "Vijana wanacheza soka la aina yake na napenda matokeo kama haya na naamini tutaendelea kuimarika zaidi.

"Unaweza kufanya hivyo mambo yakiwa shwari kabisa ndani ya kikosi. "Nina uhakika hakuna mtu anayetaka kucheza na sisi kwenye robo fainali. Itakuwa ni hatua kubwa, lakini hakuna anayetuhitaji sisi, kwani wote wanatuhofia."

Baada ya kutolewa mara nne mfululizo kwenye hatua ya 16 ya mashindano hayo, Chelsea imefuzu kwenye robo fainali kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2013-14 wakiwa chini ya kocha, Jose Mourinho.

"Sisi tunajituma kweli kweli. Na timu ikijituma sana kuna nafasi nzuri ya kupata matokeo bora.

"Ndio, tunaangalia nini kitatokea, lakini sisi malengo yetu ni kupata ushindi katika kila mchezo uliopo mbele yetu.

"Na vijana wamekuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kufanya hivyo, hivyo sina hofu yoyote.

"Lakini ni vizuri kuona kwamba timu inakuwa kwenye ubora kama huu."

## ZISIKUPITE

### ORIGI ANUKIA DORTMUND

KLABU ya Borussia Dortmund imeonyesha nia ya kutaka kumsajili straika wa Liverpool na Ubelgiji, Divock Origi mwenye umri wa miaka 25 na anaweza kupatikana kwa pauni milioni 12. (Football Insider)

### GIBBS KUTUA BROM

MLINZI wa zamani wa Arsenal na England, Kieran Gibbs, 31, amekubali kujiunga na Inter Miami mwishoni mwa msimu huu ambapo mkataba wake unafikia mwisho kule West Brom. ***(ESPN)***

### DEE BEEK AFUNGUKA

KIUNGO wa Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 23, anahisi "kupendwa" pale Manchester United , lakini anataka kuanza mechi nyingi zaidi, amesema kocha wa Uholanzi, Ronald de Boer. ***(Talksport)***

### LAPORTA, MESSI WATETA

JOAN Laporta ambaye ni rais wa Barcelona, amesema ameanza kazi ya kumshawishi nyota wa klabu hiyo Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, kubakia klabuni hapo. ***(Goal)***

### ELNENY ATAKA MKATABA

KIUNGO wa Arsenal na Misri, Mohamed Elneny mwenye umri wa miaka 28, anataka kusaini mkataba mpya na amesema hafikirii amefikia mwisho wa kuwachezea washikabunduki hao, wakati walipompeleka kwa mkopo Besiktas msimu uliopita. ***(Evening Standard)***

### RUDIGER AITAJA SPURS

KIUNGO wa Chelsea na Ujerumani, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 28, amebainisha Paris St-Germain na Tottenham zilitaka kumsajili msimu uliopita. ***(Times, subscription required)***

### DYBALA SOKONI

JUVENTUS inajiandaa kumuuza fowadi wake, Paulo Dybala raia wa Argentina mwenye umri wa miaka 27, huku Tottenham na Chelsea zote zikionyesha kumwania. ***(Star)***

### ANTONIO AKANUSHA

STRAIKA wa West Ham, Michail Antonio mwenye umri wa miaka 30, amekanusha madai kwamba, majaliwa yake yapo Jamaica, badala ya England. ***(Sky Sports)***

### DALOT ANUKIA UNITED

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anaamini mlinzi wa pembeni wa Ureno, Diogo Dalot mwenye umri wa miaka 21, bado ana nafasi pale Old Trafford msimu huo baada ya kuonyesha kiwango bora akiwa anacheza kwa mkopo AC Milan. ***(Manchester Evening News)***

### COWLEY AULA PORTS

KOCHA wa zamani wa Huddersfield, Danny Cowley mwenye umri wa miaka 43, anajiandaa kuteuliwa kuwa kocha mpya wa Portsmouth. ***(The News)***

## Mr. UK marathon kufanyika Julai

**Na Sabato Kasika**

ZAIDI ya wanariadha 2,000 kutoka ndani na nje ya Tanzania wanatarajiwa kushiriki katika mbio za Mr.UK Marathon zitakazofanyika Julai 24, mwaka huu kwenye viwanja vya Leaders Club jijini Dar es Salaam.

Mratibu wa mashindano hayo, Nelson Mrashani, aliliambia gazeti hili malengo ya mashindano hayo ni kuendelea kuhamasisha wananchi kupenda michezo.

"Mashindano haya yatakuwa ya kilomita 21 na tutakuwa na zawadi, mshindi wa upande wa wanaume na wanawake kila mmoja atapewa zawadi ya Sh. milioni moja, huku mshindi wa pili akipata Sh. 700,000," alisema Mrashani.

Mratibu huyo alitaja zawadi ya mshindi wa tatu ni Sh. 500,000 na kwamba zawadi hizo zitaendelea hadi kwa mshindi wa 10 ambaye atajinyakulia Sh. 50,000.

"Kinachoendelea sasa ni usajili wa washiriki katika mashindano hayo na mchakato huo wa usajili tutaufunga ifikapo Julai 10, mwaka huu," alisema Mrashani.

Aliongeza ada kwa ajili ya wanariadha watakaochuana katika umbali wa kilomita 21 na kilomita 10 itakuwa ni Sh. 30,000 wakati wale watakaokimbia kilometa tano watalipia Sh. 20,000.

## KVZ 'yavutwa mkia' Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LICHA ya kupoteza mchezo, Kocha Mkuu wa KVZ, Sheha Khamis, amesema bado anamatumaini ya kunyakua ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu unaoelekea ukingoni.

Akizungumza na gazeti hili baada ya kufungwa bao 1-0 na Kipanga, Sheha amesema endapo angeshinda mechi hiyo, angekuwa ameukaribia ubingwa lakini bado wataendelea kupambana ili kufikia malengo.

Kocha huyo alisema sasa hivi 'macho' yake ameyatupia katika michezo mitano iliyobaki ili aweze kufanya vizuri na kutimiza lengo lake la ubingwa kwa msimu huu.

Hata hivyo aliwataka waamuzi kuzitafsiri vyema sheria 17 za soka ili kuepusha kuchezesha kwa upendeleo katika kipindi hiki ambacho bingwa na timu zitakazoshuka daraja bado hazijajulikana.

Kwa matokeo hayo KVZ yenye pointi 30 imebakia katika nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar wakati vinara wa ligi hiyo KMKM wana pointi 32 na nafasi ya tatu inashikiliwa na Mafunzo yenye pointi 27.

# NAMUNGO FC YAENDELEA KUJIPA MATUMAINI AFRIKA

**Na Saada Akida**

LICHA ya timu yake kupoteza mechi ya pili ya hatua ya makundi ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hemed Moroco, amesema bado kikosi chake kina nafasi ya kufanya vizuri katika michezo iliyobakia na kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

**Namungo juzi ilikubali kichapo cha mabao 2-0 dhidi ya wageni Pyramids kutoka Misri katika mchezo uliofanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.**

Akizungumza na gazeti hili, Morocco alisema mechi hiyo ilikuwa na ushindani mkubwa na wachezaji wake walicheza kwa tahadhari kubwa dhidi ya Waarabu hao.

Morocco alisema wapinzani wao walitumia vyema mapungufu ya kikosi chake hasa kwenye safu ya ulinzi na hatimaye kuondoka na pointi tatu muhimu.

Alisema wachezaji wake walicheza vizuri zaidi katika kipindi cha kwanza ambapo kilimalizika kwa milango yote kuwa migumu lakini waliporejea kumalizia dakika 45 za mwisho walipunguza umakini.

"Tumetengeneza nafasi nyingi ila tumeshindwa kuzitumia vyema, pia kutokuwa na umakini katika safu ya ulinzi ilitugharimu, Pyramis walitumia nafasi hiyo kutufunga mabao hayo," alisema Morocco.

Aliongeza bado wana nafasi ya kusonga mbele kama watafanya vyema katika mechi nne zilizobakia na katika soka hakuna kukata tamaa hadi mchezo wa mwisho.

"Nadhani kupoteza mechi mbili bado hazijatuondoa kwenye mstari wetu wa kufanya vizuri na kusonga mbele katika michuano hiyo, tumeona mapungufu yetu, tutayafanyia kazi kwa ajili ya kwenda kutafuta pointi katika mechi zijazo," alisema Morocco.

Namungo FC iliyoko Kundi D itawakaribisha Nkana FC kutoka Zambia katika mechi ya mzunguko wa tatu itakayochezwa Aprili 2, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.

Timu nyingine iliyoko katika kundi hilo ni Raja Casablanca ya Morocco juzi ikiwa ugenini ilimchapa Nkana mabao 2-0.

SOKA MEZANI...




Ofisa Habari wa Kampuni ya Michezo ya kubashiri ya M-Bet Tanzania, Flora Ngahyoma (kulia), akimkabidhi mfano wa hundi mshindi wa tisa wa droo ya Perfect 12, John Puka kutoka mkoani Singida ambaye amejinyakulia kitita cha Sh. milioni 54.7 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 za ligi mbalimbali duniani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mshindi M-Bet amlilia Magufuli

**Na Mwandishi Wetu**

SHABIKI wa Arsenal inayoshiriki Ligi Kuu England na Azam FC ya hapa nchini, John Puka kutoka Singida ameshinda zawadi ya Sh. milioni 54.7 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi za ligi mbalimbali duniani kupitia mchezo wa Perfect 12 unaondeshwa na Kampuni ya M-Bet Tanzania.

Hata hivyo, Puka aliwaomba Watanzania kuendelea kukumbuka uongozi bora wa aliyekuwa Rais wa awamu ya Tano wa Tanzania, marehemu John Magufuli aliyefariki dunia juzi jijini Dar es Salaam.

Puka ambaye ni mshindi wa tisa tangu kuanza kwa mwaka huu kupitia M-Bet alisema Rais Magufuli alikuwa kiongozi shupavu aliyejali maendeleo ya nchi na hivyo tutaendelea kukumbuka.

"Pamoja na kushinda mamilioni ya M-Bet, nina majonzi makubwa ya kuondokewa na rais wetu, marehemu Magufuli. Alikuwa kiongozi wa mfano na mpaka baadhi ya nchi zilimpenda sana, naungana na familia yake katika kipindi hiki cha maombolezo," alisema Puka.

Ofisa Habari wa M-Bet, Flora Ngahyoma, alisema wanajivunia kuendelea kuwa nyumba ya mabingwa kupitia michezo yao mbalimbali ya kubashiri na anawaomba Watanzania wenye sifa kucheza michezo ya kubahatisha na kwa kufanya hivyo huku wakijua hiyo siyo ajira rasmi.

"Tunawaomba Watanzania wenye umri zaidi ya miaka 18 kuendelea kubashiri na M-Bet ili kuwa mabingwa na kubadili maisha yao. Tunajivunia kupata washindi wengi ambao mpaka sasa wamebadili maisha yao kupitia fedha za ushindi za M-Bet," alisema Ngayhoma.

Pia Ngahyoma alisema M-Bet Tanzania inaungana na Watanzania katika kipindi hiki kigumu cha maombolezo.

# Michezo

Ijumaa Machi 19, 2021

Nipashe




Timu zinaiogopa Chelsea – Tuchel UKURASA 22

# Wanamichezo, wasanii wamlilia JPM

## TFF yavunja mechi ya Stars, yasimamisha ligi zote...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

KUFUATIA msiba mzito ulioikumba Tanzania kwa kuondokewa na Rais Dk. John Pombe Magufuli, Shirikisho la Soka Nchini (TFF), klabu na wasanii mbalimbali wamejitokeza kutoa salamu za rambirambi kwa Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema kufuatia msiba huo, shirikisho lililazimika kufuta mechi ya kirafiki ya kimataifa kati ya wenyeji Harambee Stars dhidi ya Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), iliyotarajiwa kuchezwa jijini Nairobi jana.

Ndimbo alisema pia TFF imesimamisha Ligi ya Vijana chini ya miaka 20 iliyokuwa ikichezwa pamoja na Ligi ya Vijana ya umri chini ya miaka 17 ambayo ilitarajiwa kufanyika kuanzia mapema wiki ijayo.

"Mechi hiyo imefutwa kutokana na msiba wa kifo cha Rais wetu, hivyo kutokana na kufutwa mechi hiyo, Taifa Stars itaendelea kuweka kambi jijini Nairobi kujiandaa na mechi dhidi ya Equatoria Guinea."

"Umetutoka machoni mwetu, lakini sio mioyoni mwetu. Pumzika kwa amani Rais Wetu." Hivi ndivyo TFF ilivyomlilia Rais Magufuli.



Rais Dk. John Magufuli. **PICHA: MAKTABA**

### SIMBA, YANGA NI VILIO

UONGOZI wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba umesema unasikitika Rais Magufuli amefariki wakati wakiwa bado hawajatekeleza maagizo ya kuchukua ubingwa wa taji la Afrika akiwa hai.

"Umeondoka huku tukiwa hatujatimiza maagizo yako, lakini kifo chako kimekuja katika kipindi ambacho nafasi ya kutekeleza hayo maelekezo ni kubwa na uwezo huo tunao, Mh Rais wetu uliyedondoka kama ute wa mshumaa, tunakuahidi Wanasimba tutacheza mashindano haya ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa nguvu kubwa na kwa ari ya hali ya juu ili kukuenzi kwa hii changamoto uliyotuachia," alisema Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara.

Alisema Simba inawapa pole wafiwa wote na maagizo aliyoyaacha yataongoza na kuimarisha umoja ndani ya klabu yao na anaamini watayatumia maneno aliyowaambia kama msukumo wa kufikia mafanikio.

"Tangulia mwamba, tunajua na tunaamini umeliacha taifa ulilolingoza katika hali ya amani, usalama na mshikamano," Manara alimaliza.

Vinara wa Ligi Kuu Bara, Yanga wamesema wamepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Rais Magufuli na kwa niaba ya wanachama, wapenzi na mashabiki wa klabu hiyo wanatoa pole kwa Mama Samia, familia, ndugu, marafiki na Watanzania wote kwa msiba huo.

"Pumzika kwa amani Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Pombe Magufuli. Tutakukumbuka milele daima. Pumzika kwa amani, daima mbele nyuma mwiko," ilisema taarifa ya Yanga.

Mabosi wa Azam FC nao wameeleza kushtushwa na taarifa za kifo cha kiongozi huyo mkuu wa nchi.

"Azam FC, tunaungana na Watanzania wote kuomboleza kifo cha mpendwa wetu, kwa kutambua na kuheshimu mambo makubwa aliyohudumu ndani ya serikali. Tunaomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi." Ilimaliza taarifa ya Azam kwenye mtandao wake rasmi wa kijamii.

"Hakika sisi ni wa Mungu na kwake tutarejea. Pumzika kwa amani Mh. John Magufuli." Uliandika mtandao rasmi wa klabu ya Mtibwa Sugar ya Manungu, mkoani Morogoro.

Biashara United ya Mjini Musoma pia wametoa salamu za rambirambi kufuatia msiba huo mzito na kuwataka Watanzania kuzidi kumwomba Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi.

"Pumzika Rais wetu, tutakukumbuka daima." Ilikuwa na kauli ya Coastal Union ya jijini Tanga.

Pia timu za soka za wanawake zikiongozwa na mabingwa watetezi, Simba Queens, Fountain Gate, Yanga Princess zimetuma salamu za pole kwa Watanzania wote.

### CHANETA, NGUMI WAOMBOLEZA

Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA), kimetoa salamu za rambirambi kufuatia msiba wa rais huyo wa awamu ya tano.

Mwenyekiti wa CHANETA, Devotha Marwa, alisema Rais Magufuli alifanikiwa kuweka kipaumbele katika kila mchezo kwa kuwataka mawaziri husika kwenye sekta hiyo kuhakikisha michezo yote inakuwa imara.

"Tunasikitika, tumepata msiba mzito. Hatuwezi kuuelezea kutokana na upendo wake. Hakujali chochote na mara kadhaa kwa upande wetu CHANETA tumekuwa tukienda kwenye ofisi yake kwa ajili ya ushauri na kusaidia," alisema Marwa.

Shirikisho la Ngumi za Ridhaa (OBFT), mbali na kushtushwa na taarifa hiyo, limesema limebaki na simanzi kwani alikuwa ni kiongozi aliyeipa kimaumbele michezo.

Katibu Mkuu wa OBFT, Lukelo Willilo, alisema Tanzania imepata pigo kubwa kwa msiba huu uliotokea.

"Ni pigo kwetu, maana ameondoka kabla hajakamilisha mipango yake, ila ni kazi ya Mungu, hivyo tunatakiwa tumuenzi na hakuna njia nyingine ya kutekeleza kile ambacho alikiahidi kwenye michezo, ikiwamo kuzisaidia timu za taifa za michezo yote," alisema katibu huyo.

Mwekezaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Simba, Mohamed Dewji 'Mo' naye ameandika; "Mimi na familia yangu tumehuzunika sana na taarifa za kifo cha Rais wetu mpendwa Dk. John Magufuli. Tunatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa ujumla kwa msiba huu mzito. Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake mahali pema peponi." Aliandika Mo.

Nahodha wa Simba, John Bocco amemtaja Rais Magufuli alikuwa ni kiongozi aliyetanguliza mbele maslahi ya taifa na si ubinafsi.

"Kweli kizuri hakidumu, kwaheri mzalendo wa kweli. Mtanzania uliyeiweka Tanzania mbele na si ubinafsi. Naamini wa kujifunza tumejifunza mengi sana kutoka kwako na wakuona, tumeona mengi na mazuri kutoka kwako. Wewe ni zaidi ya somo kwa Watanzania," alisema Bocco.

Luis Miquissone alitoa pole kwa msiba na kusema Watanzania wamepoteza kiongozi bora na imara.

Rais wa Shirikisho la Soka Kenya (FKF), Nick Mwendwa naye pia ametuma salamu za pole kwa Watanzania.

Mwimbaji mkongwe wa muziki wa taarabu nchini, Khadija Kopa alisema msiba uliotokea ni pigo kwa wananchi wote kwa sababu tangu Rais Magufuli alipoingia madarakani utendaji kazi ulifanyika kwa weledi.

"Alikuwa mchapakazi, alibadilisha kila idara, akili za wafanyakazi zilichangamka, kila jambo lilionekana jepesi, alikuwa jasiri, alijiamini, hatukuwa tena na mawazo, hata tukiumwa hatuhangaiki, bima zilitusaidia," Kopa alisema hayo huku akitokwa na machozi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042